TRUTH CENTERED TRANSFORMATION

MODULE

MASUALA YA KIFEDHA

MWONGOZO WA MWALIMU

Truth Centered Transformation—Module: Money Matters v3.2. Copyright ©2018 Reconciled World, Phoenix, Arizona, United States of America. www.reconciledworld.org

Kazi hii inatolewa chini ya Creative Commons Attribution–ShareAlike 3.0 license. Unaruhusiwa na kuhamasishwa kubadilisha kazi kunukuu, kusambaza na kuituma kwa ukizingatia yafuatayo:

Utambuzi – Lazima uitambue kazi hii kwa kutaja rejea zifuatazo: Copyright ©2017. Imetolewa na Reconciled World (www.reconciledworld.org), chini ya Creative Commons Utambuzi–ShareAlike 3.0 license. Kwa taarifa zaidi , uangalie tovutiwww.creativecommons.org.

Si kwa biashara – Huwezi kutumia kazi hii kibiashara

Ukitaka kuitafsiri wasiliana na info@tctprogram.org.

Mistari yote ya Maandiko Matakatifu inatokana na Biblia, New International Version®, NIV®. Copyright ©1973, 1978, 1984, 2011 by Biblica, Inc.TM. ikitumika kwa ruhusa ya Zondervan. Haki zote zimehifadhiwa dunia nzima. www.zondervan.com. The “NIV” and “New International Version” are trademarks registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc.TM.

Kabla hujaanza

Angalizo muhimu kwa Moduli hii inayohusu Masuala ya Kifedha

Katika Moduli hii, kuna Tafakari pamoja na Masomo. Tafakari hizo zimeandaliwa ili kuwa na muda wa kutafakari kwa ufupi kabla ya kuanza masomo kama ilivyo kawaida.

Unapohusisha na mazingira yako ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo:

- Ni vizuri kuzibaini chagamoto zinazolikabili suala zima la Utoaji pamoja na Zaka.
- Ujue lugha ya Kifedha inayotumiwa:
  - Tarakimu zilizotumiwa
  - Dola zimetumiwa katika mwongozo huu lakini zinaweza kubadilishwa kulingana na mazingira ya watu wako.

Maelekezo kwa Mwalimu: *Chukua muda kupitia bajeti za na idadi inayotumiwa kulingana na watu wa mazingira unayotumika. Kuna Ukrasa wa Mahesabu (Excel) ulioandaliwa ili kukurahisishia kazi hii.*

Kujiandaa Kufundisha Somo

1. Soma **Kiongozi cha Mwalimu** kwa uangalifu, mara nyingi iwezekanavyo. Sisitiza au andika notisi pembeni mwa karatasi kujikumbusha pointi za muhimu.
2. Angalia **mawazo makuu** kwa kila kipindi ili ujue wanafunzi watajifunza nini katika somo.
3. Soma aya zote za Biblia kabla.
4. Angalia kuona ni **vifaa** gani vinahiyajika katika kila somo na kuhakikisha unatengeneza nakala za handout na kutengeneza vionyeshi ambavyo vinatumika katika somo hilo.
5. Hakikisha unaelewa kila **shughuli** katika somo (maigizo, michezo, vionyeshi). Unaweza kuifanyia mazoezi pamoja na familia au marafiki zako.
6. Chukua muda **kuomba** ili Mungu aandae wanafunzi, wanafunzi wasikie kile Mungu anachotaka wasikie na Akusaidie kufundisha vitini. Kumbuka kwamba ni kwa nguvu ya Mungu tu kwamba tutaweza kuwabadilisha watu.

Jinsi ya kutumia mwongozo huu wa Mwalimu

1. **Mawazo Makuu na Vifaa:** Kila somo huanza na sehemu hii.
   a. **Mawazo Makuu**–Kuna mawazo mengi mazuri katika kila somo, lakini washiriki lazima waelewe mawazo haya makuu ifikapo mwisho wa kila somo. Ni vizuri kujiuliza kama unadhani washiriki wanaweza kukumbuka mawazo haya mazuri baada ya kuongoza somo. Rudia mara kwa mara mawazo makuu ili iwasaidie kukumbuka.
   b. **Vifaa** – Orodhesha vifaa maalumu vinavyohitajika kwa kila somo ikiwa ni pamoja na Vielelezo na Vitini vya Masomo vya wanafunzi. Mwongozo huu wa Mwalimu utaonyesha jinsi ya kutumia vifaa hivyo:
      - **Miongozo ya Mwanafunzi** – Utaona alama kama unayoiona hapo upande wa kulia wa ukrasa huu kwenye Ukrasa wa Mwongozo wa Mwanafunzi pale unapohitajika kutumika.
      - **Vionyeshi** –Utaona alama upande wa kushoto wa Ukrasa wa Mwongozo wa Mwanafunzi kila unapohitajika kutumika.

Sehemu ya 1: Masomo ya Tafakari

Tafakari ya 1: Mtazamo wa KiBiblia kuhusu ya fedha- Sehemu ya 1

Mawazo Makuu

- Fedha isiwe lengo letu kuu
- Tunapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kujiingizia kipato tuweze kuzihudumia familia zetu pamoja na watu walio na uhitaji.

Vifaa

- Mwongozo wa Mwanafunzi: Tafakari ya 1 (kwa Kila mshiriki)

Utangulizi

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

- Unajua mistari ipi ya Biblia inayozungumzia fedha?
- Ni kanuni zipi twaweza kujifunza kuhusu fedha kutokana na vifungu hivyo?
- Unadhani Mungu anahusika juu ya matumizi yetu ya fedha?
- Je, kuonekana kuwa ni mtu wa Kiroho sana kunadhirishwa na kuwa tajiri au maskini?

Biblia inazungumza mambo mengi juu ya fedha. Kuna aya nyingi za Biblia zinazozungumza kuhusu fedha kama ilivyozungumza juu ya maombi na Imani.Mungu mwenyewe ameona kuwa Mada hili ni muhimu na inapaswa kuzungumzwa.Fedha ina uwezo wa kutusaidia sisi lakini pia inaweza kutuangusha.Mara kwa mara tumetumia muda mwingi kushughulika na fedha.Tunapaswa kujifunza jinsi ya kutumia fedha katika njia zinazomtukuza Mungu.

Mtazamo wetu mkuu usijengwe katika fedha

KIKUNDI KIDOGO CHA MJADALA

Maelekezo kwa Mwezeshaji: *Gawanya* ***miongozo wa Mwanafunzi****: Tafakari ya* ***1****. Katika vikundi vidogo vya washiriki 3-4 waipitie mkwa makini nusu ya kwanza ya handout, kisha walete taarifa.*

Soma: Mathayo 6:19-24; 33

Kifungu hiki ni sehemu ya "Mahubiri ya Yesu akiwa Mlimani au Hotuba Mlimani.Katika hotuba bii, Yesu anaongea na wanafunzi wake akiwaambia kuhusu Maisha katika ufalme wa Mungu.

- Je, katika aya hizi ztunajifunza nini juu ya fedha?
- Nini maana ya kuzitumikia fedha?
    - *Ni pale tunaporuhusu fedha zitutawale na kututumikisha na hii hutokea hasa wakati tunaposhughulika kuzitafuta, ili kujikusanyia fedha nyingi zaidi.*
- Je, hii inamaanisha kwamba hatupaswi kamwe kuwaza juu ya fedha?
    - *La, si hivyo, tunapaswa kuwaza juu ya fedha lakini tusiirihusu fedha kututawala sisi na kututumikisha. Tunapaswa kuwa mawakili walio na hekima.*
- Je, nini maana ya kujiwekea hazina mbinguni? Tunawezaje kulifanya jambo hili?
- Mafundisho ya Yesu yanatofuautianaje na utamaduni wetu?
- Je, kifungu hiki kinatuhimiza kuelekeza mtazamo wetu wapi?

Soma: 1Timotheo 6:6-11.

- Mtazamo wetu kuhusu fedha unapaswa kuwa wa namna gani?
    - *Ikiwa tuna fedha nyingi na mavazi mengi tunapaswa kuridhika.*
- Kwa nini kupenda zaidi fedha ni jambo lenye hatari?
    - *Ni rahisi kutenda dhambi au viendo viovu kwa lengo la kujipatia fedha.*
    - *Inaondoa moyo wa kuwa wakarimu badala yake tunakuwa wabahiri na wachoyo.*
    - *Ni rahisi mno kumkana Mungu, kutokuifanya kazi yake, na kutokuwapenda wenzetu.*

REJESHA RIPOTI

Kama vile tulivyojifunza, hatupaswi kupenda mno fedha. Baada ya kufariki dunia, kamwe hizo fedha na mali hatutakwenda nazo. Jambo la muhimu na tunalopaswa kukumbuka ni kwamba, haijalishi wingi wa fedha tulizo nazo bali jambo la msingi ni kujiuliza, Je, sisi ni Wakristo, na ikiwa sisi ni wakristo, je tunatumiaje fedha zetu? Mtazamo wetu katika maisha usijengwe katika fedha, bali hasa uwe katika kumtukuza Mungu.

Kazi ni kitu chema

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Muda mwingine tunaposhindwa kuelewa mafundisho ya Biblia juu ya fedha, matokeo yake tunajikuta tukiamini kuwa fedha na kazi ni vitu vibaya. Tunapaswa kufanya kazi kwa bidii, lakini siyo kwa lengo la kujipatia fedha zaidi kwa manufaa yetu binafsi. Tukifanya kazi kwa lengo la kujipatia fedha zaidi, basi huo ni ulafi. Tunapaswa kufanya kazi kwa bidii lakini siyo kwa lengo la kujikusanyia fedha zaidi kwa manufaa yetu binafsi.

Soma: 2 Wathesalonike 3:6-15.

Mtume Paulo alipata shida kuhusu Wakristo wa Kanisa la Thesalonike kuwa walikuwa hawafanyi kazi yoyote.

- Mtazamo wa Mtume Paulo kuhusu kufanya kazi ulikuwa ni upi?
- Kwa nini alichagua kufanya kazi kuliko kutumia muda mwingi kufundisha Wakristo kanisani?
- Mtume Paulo alisema ni nini kingetokea kwa wale watakaokataa kufanya kazi kwa bidii?

Soma: 1 Timotheo 5:8.

- Je, Mtume Paulo anafundisha nini juu ya utunzaji wa familia zetu?
- Unadhani ni kwa nini alitumia maneno makali?
    - *Mtume Paulo alikuwa akiwaonya kwa ukali wale walioshindwa kuzihudumia familia zao. Mungu hakutuumba tukae tu bila kufanya kazi bali alitupatia jukumu la kuwasaidia wasiojiweza ikiwa ni pamoja na kuzitunza famila zetu. Mtume Paulo hajazungumzia wale wanaofanya kazi kwa bidii na kutunza familia zao vizuri, bali kwa wale wazembe wanaotumia muda wao mwingi kwa mambo mengine na kisha wakasahau kuzihudumia familia zao.*

Soma: Waefeso 4:28.

- Mtume Paulo anazungumza nini kuhusu kazi?
- Kwa nini tunagizwa kufanya kazi?
    - *Mtume Paulo aliwatia moyo Waefeso juu ya kufanya kazi kwa bidii ili waweze kuwasaidia wengine walio na uhitaji.*

Kama watu wa Mungu, tumeagizwa kufanya kazi kwa bidii. Tunapaswa kutumia ujuzi wetu tulio nao ili kujitengeneza kipato kwaajili yetu sisi binafsi, watu wenye uhitaji, wakristo wenzetu na maskini pia. Wakati kuipenda fedha ni jambo ovu, bali kuithamini familia pamoja na watu wengine, ni jambo linalomtukuza Mungu.

Soma: Mwanzo 2:2.

- Je, nani alikuwa mtu wa kwanza kufanya kazi?
- Je, mfano wa Mungu katika kufanya kazi una maana gani kwetu sisi?
    - *Mungu alikuwa wa kwanza kufanya kazi. Biblia inasema kuwa tumeumbwa kwa mfano na sura ya Mungu.Maana yake ni kwamba, tumeumbwa ili tufanye kazi pia.Ikiwa tutafanya kazi kwabidii, tunaonyesha kumheshimu na kumtii Mungu na ndipo tunapomwiga Mungu.*

Soma: Mwanzo 2:15, 18.

- Kwa nini Mungu alimweka mtu bustanini?
- Kwa nini Mungu alimuumba mwanamke?
    - *Mungu alimweka mtu bustanini ili ailime na kuitunza.Mapema katika aya ya 18, Mungu anasema , si vizuri mtu huyu awe peke yake katika kazi yake bali alimuumba mwanamke ili awe msaidizi mkuu wa mwanamme.Hii inamaanisha kuwa, wote waliumbwa kwa lengo la kufanya kazi ingawa kuna majukumu na nyajibu mbalimbali kwa kila mmoja.*

Soma: Kutoka 20:8.

- Je, tunapaswa kufanya kazi kwa siku ngapi?
- Je, tunapaswa kupumzika kwa siku ngapi?
    - *Hatupaswi kuutumia muda wetu kwa kukaa bila kufanya kazi wala hatupaswi kuutumia muda wetu wote kufanya kazi bila kupumzika hata siku moja kwa wiki.*
    - *Wakati Mungu alipotoa amri hizi, alikuwa akizungumza na watu waliokuwa wakipata fedha zao kutokana na shughuli za kilimo. Ingawa wakati mwigine tunaonekana hatuna kazi yoyote ya kufanya, na wakati mwingine tunaonekana kuwa na mambo mengi hata kushindwa kupumzika, bado tunapaswa kumheshimu Mungu kwa kujitoa muda wetu pia.*

TAFAKARI

Tumia Dakika 2 kutafakari juu ya maswali yafuatayo:

- Je, unatii agizo la Mungu kuhusu swala zima la kujipatia fedha?
- Je, ni hatua zipi za Mabadiliko ungependa kuchukua?

JADILI PAMOJA NA MWANAKIKUNDI MWENZAKO

Jadili kwa pamoja maswali yafuatayo mkizingatia maisha yenu binafsi na kisha kila mmoja aombe kwaajili ya mwenzake. Maswali yameorodheshwa kwenye kitini chako.

Fedha isiwe lengo letu kuu: Jiulize maswali haya:

- Je, ninapenda mno fedha? Je, ninatumia muda wangu mwingi kuwaza jinsi ya kujipatia fedha zaidi?
- Je, niko radhi na vile nilivyonavyo?
- Je, ninajiwekea hazina mbinguni au duniani?

Kazi ni kitu chema:

- Je, ninafanya kazi kwa bidii?
- Je, ninauwezo wa kuihudumia familia yangu?
- Je, kuna wahitaji gani katika jamii yetu? Tunawezaje kuwahudumia mmoja mmoja na kama kikundi?

Tafakari ya 2: Mtazamo wa Kibiblia juu ya fedha: Sehemu ya 2

Mawazo Makuu

- Mungu ameahidi kutupatia mahitaji yetu yote. Ikiwa tunapungukiwa mahitaji yetu ya kawaida, basi tunapaswa kujiuliza kwa nini hali hiyo inatupata.
- Tunapaswa kutumia fedha zetu kwa hekima.

Vifaa

- Mwongozo wa Mwanafunzi: Tafakari 2 (Moja kwa kila Mshiriki)

Utangulizi

KIKUNDI KUKUBWA CHA MJADALA

Tumejifunza kwamba fedha isiwe ndilo lengo letu kuu na kuwa tunapaswa kufanyakazi kwa bidii ili tuweze kujipatia kipato cha kutosha kwaajili ya familia zetu na kuwasaidia maskini.

- Je, Biblia inatufundisha nini zaidi kuhusu fedha?
- Je, kuna ahadi zipi zinazotutia moyo sisi tunapofanyakazi kwaajili ya kutunza familia zetu na kuwasaidia maskini?

Hetu tuangalie jinsi Mungu alivyoahidi kutupatiaa mahitaji yetu na jinsi anavyotarajia kutuona tukitumia vizuri fedha zetu.

Mungu ameahidi kutupatia mahitaji yetu

Soma: Mathayo 6:25-33.

Katika aya hizi tunjifunza kuwa Mungu ameahidi kutupatia mahitaji yetu ikiwa tutamtanguliza Yeye kwanza. Biblia pia inaeleza sababu za sisi kutokuwa na mahitaji ya kutosha. Tutaangalia mambo haya sasa.

KUKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Maelekezo kwa mwezeshaji: Gawanya Mwongozo wa Mwanafunzi*: Tafakari ya 2. Kila kundi lisome fungu la Mistari na kuorodhesha mawazo makuu yanayopatikana ndani ya vifungu hivyo. Ikiwa wana muda waziada wanaweza pia kuangalia mistari mingine. Kama huna Miongozo ya Wanafunzi, basi gawa mistari kwa kila kikundi - ispokuwa usiwagawie Mawazo makuu.*

Kwa nini tunajikuta hatuna fedha za kutosha:

- **Uvivu** – Mithali 10:4, 13:4; 24:30-34.
    - *Tunapaswa kuhakikisha tunafanya kazi kwa bididi bila kukaa tu*
- **Tamaa/ Ulafi** – Mithali 28:25
    - *Mungu hajatuahidi utajiri bali utoshelevu. Je, kweli tunaupungufu au hatujaridhika na kile alichotupatia?*
- **Kupenda anasa** – Mithali 21:17; 23:20-21
    - *Anasa hizi zaweza kuwani vitu vidogovidogo kv. Sigara, Pombe, vyakula vizuri, nk.Hebu tafakari jinsi unavyotumima fedha zako-. Je, ni katika anasa au ni vitu unavyohitaji?*
- **Uchoyo**– Mithali 11;24
    - *Je unatoa kama Mungu alivyoagiza? Mungu ametuambia katika Neno lake kwamba tusipomtolea hawezi kutubariki.Yeye hutubariki kulingana na kiwango chetu cha utoaji.*
- **Upumbavu**– Mithali 3:13-16
- **Kutokutii** –Mithali 28:13, 2 Nyakati24: 20

REJESHA RIPOTI

Melekezo ya Mwezeshaji: *Wanavikundi washirikishane juu ya mambo waliyojifunza. Kumbuka kuwa kikundi kikubwa kinapaswa kurejesha sababu sita kwanini tunakumbana na uhaba wa kifedha.*

Sababu nyingine inayosababisha tujikute katika uhaba wa kifedha ni kukosekana kwa haki. Omba msaada wa Mungu. Mungu ni rafiki wa wale wanaoonewa na kukoswa haki.

Kama unajikuta katika uhaba wa mahitaji na kudhani kuwa Mungu ameshindwa kukupatia mahitaji yako yote, hebu tafakari juu ya maisha yako kulingana na maeneo yaliyoorodheshwa hapo juu. Mwombe Mungu kuonyeshe hatia uliyo nayo moyoni, Tubu na umwombe Mungu akusamehe na kukusaidia kubadilika.

- Je, kati ya sababu zote unadhani ni ipi inayoonekana sana katika eneo lako? Unadhani ni kwanini?
- Je, kuna njia za kuzuia hali hiyo katika maisha yetu binafsi? Na maisha ya wengine?
- Je kuna Sababu nyingine unazodhani kuwa zinaweza kusababisha hali hiyo?
- Je, tunawezaje kuitia moyo Familia ya jirani kwamba Mungu ameahidi kutupatia mahitaji yetu?

Utumiaji wa fedha zetu binafsi

MJADALA KATIKA KIKUNDI KIKUBWA

Soma Mathayo 25:14-30.

Kupitia mfano huu, Mungu anatufundisha jinsi yakuwa mawakili wema wa mali yote alivyotupatia. Bwana aliyekwenda safari ni picha ya Mungu na fedha aliyowapatia watumishi wake in picha ya fedha na vipawa alivyotupatia Mungu.

- Je, watumishi wake wote walipokea kiasi kile kile cha fedha?
- Ni jambo gani lilitokea kwa mtumishi wa kwanza?
- Ni jambo gani lilitokea yule mtumishi wa mwisho? Kwa nini mmliki wa shamba alichukia?
- Je, hadithi hii inatufundisha nini sisi?

Si kwamba kila mmoja wetu tumepewa kiwango sawa na mwenzake. Mungu hatatuhukumu kwa wingi wa vile alivyotugawia bali atatuhukumu kulinga na vile tunavyovitumi vile alivyotupatia. Mungu anatajarajia kutuona tukizitumia kwa hekima zawadi alizotupatia badala ya kuzitapanya ovyo (1Timotheo 5:8) na kwaajili ya maskini(Waefeso 4:28).

PAMOJA NA MWENZI

Jadili kuhusu maisha yenu biafsi na kisha kila mmoja amwombee mwenzake.

- Je, huwa tunazitumia fedha zetu kwa hekima?
- Je, ni kwajinsi gani tunaweza kuzitumia kwa hekima?

Tafakari ya 3: Makosa makubwa yanayofanywa katika utumiaji wa fedha Sehemu ya 1

Mawazo makuu

Kuna makosa makubwa, wakati wa kutumia fedha. Tunahitaji kujifunza jinsi ya kuyaepuka. Makosa hayo ni haya yafuatayo:

- Kamwe siwazi juu ya fedha zangu.
- Kama nikiwa nazo, nitazitumia!
- Sina fedha za kutosha
- Siwezi kusubiri, hivyo lazima nikakope.

Vifaa

- Mwongozo wa Mwanafunzi: Tafakari ya 3 (Mwongozo mmoja kwa kila kikundi kidogo)

Maelekezo kwa mwezeshaji: Hizi ni tafakari zilizoandikwa kwa ufupi sana yaani sehemu ya 1 na ya 2. Muda mwingine ikiwa unaendesha mafunzo kwa muda wa siku kama 3 hivi, hizi tafakari zinapaswa kuunganishwa pamoja ili kuwa tafakari ndefu.

Utangulizi

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

- Ni kanuni zipi za msingi tulizojifunza kuhusu fedha?

Hebu sasa tuangalie makosa 4 kati ya 8 yanayofanywa na watu juu ya matumizi ya fedha.

- Unadhani ni makosa yapi makubwa zaidi?

Kosa 1: Kamwe siwazi kuhusu fedha zangu

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Soma Luka 12:42-47.

- Je, Bwana alitarajia kuona watumishi wake wamefanya nini?
    - *Bwana alitarajia kuwaona watumishi wake wako macho kusimamia watu au vitu vilivyokuwa chini ya usimamizi wao kwa hekima na kutenda kulingana na vile alivyokusudia.*

Kila kitu ni Mali ya Mungu.Fedha tulizo nazo tumepewa zawadi kutoka kwa Mungu.Ametupatia ili tuzi, tumie kwa hekima. Tunapaswa kuwa na matumizi mazuri ya fedha, hasa tukitambua kuwa ni maliya Mungu na anatarajia kutuona tukizitumia vizuri.

Kosa la 2: Kama nikiwa na fedha, nitazitumia

MADALA KATIKA KIKUNDI KIKUBWA

Soma: Mithali 21:20

- Mithali hii inafundisha nini kuhusu wale wanaotumia vyote walivyonavyo?
- Je mtu aliye na hekima hufanya nini?
    - *Hujiwekea akiba mafuta na chakula.*
- Je, ni mambo gani tunajifunza kutokana na Mithali hii?
    - *Hatupaswi kutumia na kumaliza vyote tulivyonavyo, badala yake tunapaswa kutunza*

Soma Mhubiri 2:10-11.

- Je, mtu huyu alitumiaje fedha?
- Ilimwongezea furaha yoyote?
    - *Mtu huyu tunayesoma habari zake katika kitabu hiki cha Mhubiri, alizitumia vibaya fedha lakini bado hakuwa na furaha?*

Fanya mjadala:

- Nijambo gani hutokea kipindi tunapopata fedha na kuzitumia zote wakati huohuo?
- Je, umewahi kukutana na hasara iliyotokana na matumizi ya fedha ambayo hukuwa na bajeti yake? Je, unaweza kusimulia ushuhuda wowote?
- Je, umewahi kununua kitu flani ulichokuwa ukikitamani, lakini bado ukajikuta kuwa hakijakuongezea faida yoyote?
- Tunawezaje kujiepusha na tatizo hili?

Kosa la 3: Sina fedha za kutosha

KIKUNDI KIDOGO CHA MJADALA

Maelekezo kwa Mwezeshaji:

*Gawanya washiriki wako vikundi vya watu 3-4. Gawanya **miongozo ya wanafunzi**: Tafakari ya 3. Kila kikundi kijadili kosa moja na kuchambua mawazo makuu yanayopatikana.*

Soma: Wafilipi 4:11-12.

- Nini maana ya kuridhika?
- Je, ni katika mazingira yapi mtume Paulo alikuwa ameridhika?
- Je, tuko radhi na Mali tulizonazo?
- Ikiwa tuko radhi, inamaanisha kwamba tunapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kujipatia kipato? Tazama: Mithali 23:4-5 na Mithali 24:33-34.
    - *Tunapaswa kuwa waangalifu wakati wa kujibu swali hili. Tunapaswa kujiepushe na Uvivu, bali tufanye kazi kwa bidii ili tuweze kuzihudumia familia zetu. Mithali 24 inatukumbusha kuwa kama sisi ni wavivu tutaendelea kuishi katika hali ya umaskini na uhaba katika kila. Kwa hiyo, tunapaswa kuwa waangalifu tusije tukasahau kuzihudumia familia zetu, wal kuukat wajibu wetu kwa Kanisa kwa kigezo cha kutafuta utajiri. Mithali 23 inatukumbusha kwamba tusiwe na tamaa ya kuupata utajiri.*

Kuridhika ni jambo la muhimu mno katika maisha. Njia moja ya kuipata tabia hii, ni kumshukuru Mungu kwa kila kitu alichotupatia. Kama Paulo anavyosema amejifunza kuridhika, hivyo nasi tunapaswa kujifunza kuridhika katika mazingira yoyote tuliyonayo.

Kosa la 4: Siwezi kusubiri, lazima nikope

KIKUNDI KIDOGO CHA MJADALA

Soma Mithali 22:7.

- Madhara ya deni ni nini?
- Ni baadhi ya vitu gani ambavyo watu huingia katika madeni ili kuvinunua?
- Ni njia ipi nyingine inayoweza kusaidia kupata vitu tunavyovihitaji?
    - *Kutunza fedha*

Wakati mwingine tunataka kuwa kitu flani wakati huohuo, tunaamua kukopa fedha ili kupata kitu hicho. Kwa mfano, familia hununua TV na vitu vingine kwa kutumia madeni. Hii haionyeshi utumiaji mazuri wa madeni. Deni ni mtego. Tunahitaji kuwa mvumilivu na kutunza akiba kwaajili ya vitu tunavyohitaji. Deni inapaswa

kutumika tu katika nyakati za matatizo ya mara chache, au kununua vitu vitakavyotuongezea mapato ya ziada. Tunahitaji kuhakikisha kwamba deni ni la haki na na kwamba tumeweka utaratibu wa wazi wa malipo ambao tutaufuata katika kulipa deni hilo. Kuwa mvumilivu mpaka uweze kumudu gharama ya kitu akitu chochote unachokipenda. Tutajifunza zaidi kuhusu madeni katika somo jingine hapo baadaye.

REJESHA RIPOTI

PAMOJA NA MWENZA

Ukiwa na mwenza, jadili kila moja ya makosa 4.

- Ni koza lipi kati ya haya linalokusumbua zaidi?
- Je, ni hatua ipi unayopaswa kuitumia ili kuepukana na kosa hilo?

Tumieni muda huo kuombeana kila mmoja juu ya kupambana na kuepukana na makosa 4 juu ya fedha.

Tafakari Ya 4: Makosa Makuu juu ya Matumizi ya Fedha zako sehemu ya2

Mawazo makuu

Kuna makosa ya wazi wakati tunapotumia fedha zetu. Inabidi tujifunze mbinu za kuepukana nayo. Makosa hayo ni haya yafuatayo:

- Ninatumaini kuwa na fedha nyingi kama wengine
- Mimi ni maskini sana katika utoaji
- Daima ninamashaka kuhusu fedha zangu
- Ninajiingizia fedha na kuzitumia kwa njia zisizomheshimu Mungu

Vifaa

- Mwongozo wa Mwanafunzi: Tafakari ya 4 (1 kwa kundi dogo)

Utangulizi

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

- Ni makosa yapi manne ambayo watu hufanya wakati wa kusimamia fedha?
    - *Kamwe siwazi juu ya fedha zangu.*
    - *Kama nikiwanazo, ninazitumia*
    - *Sina fedha za kutosha*
    - *Siwezi kusubiri, lazima nikakukope*
- Elezea jinsi kujifunza mafundisho haya kumeathiri matumizi yako tangu tafakari iliyopita.

Sasa tutaangalia makosa mengine 4 ambayo watu hufanya wakati wa kusimamia fedha zao.

Kosa la 5: Ninatamaini kuwa na fedha kama watu wengine

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Soma Kutoka 20:17 na Luka 12:15.

- Nini maana ya kutamani?
- Kitu kipi kinatuzuia? Kwa nini?

Soma: Mhubiri 5:10.

- Je, mtu mwenye tamaa ya fedha amewahi kujisikia kuwa anazo za kutosha?

Hupaswi kuruhusu tamaa na ulafi viujaze moyo wako. Kupenda fedha kumaanisha kwamba, haijalishi tumekuwa matajiri kiwango kipi, bado tutajisikia kuhitaji fedha zaidi. Muda mwingine tunawaonea wivu lwe walio na fedha nyingi. Shetani hutudanganya kuwa, fedha na mali hutufanya tuwe wenye furaha. Kwa mfano- “Kama nitapata PikiPiki, maisha yangu yatakuwa mazuri zaidi.” Mali hazitaweza kutuletea furaha. Zinaweza kutufanya sisi tujisikie furaha kwa muda mfupi tu, na baadaye tunaanza kutamani kitu kingine tena.

- Je umesha wahi kununua kitu ulichokuwa ukikihitaji mno? Je, ulijisikiaje baada ya miezi 6 au mwaka?
- Je, kuna kitu chochote ulichokuwa ukikitamani wakati uliopita? Je, ni jinsi gani unaweza kuacha tabia hiyo na kuridhika na vile ulivyonavyo?

Kosa 6: Mimi ni maskini sana katika utoaji

KIKUDI KIKUBWA CHA MJADALA

Maelekezo kwa Mwezeshaji: *Wagawanye washiriki kwenye vikundi ya watu 3-4. Sambaza* ***mwongozo wa Mwanafunzi****: Tafakari ya 4. Kila kikundi kinapaswa kujadili kosa moja, kisha kufupisha wazo kuu linalopatikana.*

Soma 2 Wakorintho 8: 1-5.

- Je, aya hii inasemaje kuhusu kutoa katika nyakati uhitaji.
- Tunawezaje kumtia moyo kila mtu kutoa bila kujali mazingira yake?

Mungu akubariki kila unapotoa.

Soma Malaki 3:10-12.

- Tunapaswa kufanya nini kutokana na Msitiari huu?
- Ni nini kitatokea ikiwa tutafanya?

Hii ndiyo sehemu pekee katika Biblia ambayo Mungu anatuambia tumjaribu kwa njia ya kumtolea. Anatuambia wazi kuwa kama tukileta zaka zetu kamili, Yeye atatubariki. Tena na tena, Biblia hutukumbusha kuwa kiasi kilekile tunachomtolea Mungu, ndicho Mungu atakachturudishia sisi.

Kosa la 7: Daima ninamashaka na fedha zangu

KIKUNDI KIDOGO CHA MJADALA

Soma Mathayo 6: 25-34.

- Je, Mungu anasema nini kuhusu kuwa na mashaka?
- Kwa nini anatuambia kuwa tusiwe na mashaka?
- Badala yake tuwaze kuhusu nini?
- Tunawezaje kuondokana na mashaka?
- Je, umwahi kuwepo wakati wa kuwa na mashaka?

Mungu hataki tuwe na mashaka kuhusu fedha. Wakati tunahitaji kuwa na hekima na umakini katika swala zima la utumiaji wa fedha, hatupaswi kuruhusu masaha yatutawale. Mwombe Mungu akuepueshe na mashaka na kukusaidia kumsheshimu kwa kile alichokupatia.

REJESHA RIPOTI

Kosa la 8: Ninapata fedha na kuzitumia katika nji zisizomtukuza Mungu

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Soma Ezekieli 22:12-14.

- Je, kutokana na mistri hii ni njia ipi mbaya inaelezwa ambayo tunaweza kuitumia kupata na kutumia fedha zetu vibaya?
- Je, ni matokeo yapi ya kupata na kutumia fedha zetu katika njia isiyomheshimu Mungu?

Bibilia inatuagiza kumheshimu Mungu katika kila kitu tunafanya na hiyo inajumuisha jinsi tunavyopata na kutumia fedha. Hatupaswi kutoa wala kupokea rushwa au mapato ya udhalimu, kuiba wala kudanganya, maana tutavuna kile tunachopanda.

PAMOJA NA MWENZAKO - Ukiwa pamoja na mwenzako, tafakari kila moja ya makosa hayo manne (4)

- Je, ni lipi kati ya haya makosa Manne (4) bado unajikuta unalirudia mara kwa mara?
- Je, unaweza kuchukua hatua gani ili kuepuka kufanya kosa hili?
- Je, ni baadhi ya mabadiliko yapi ya kivitendo utaenda kufanya katika njia ya kupata na kutumia fedha zako?

Omba kila mmoja kuhusu mabadiliko ambayo unataka kuchukua ili kuepuka kufanya makosa sawa.

Tafakari ya 5: Utoaji na Zaka

Mawazo makuu

- Mungu hupenda tumtolee.
- Hata waliomaskini wanapaswa kumtolea.
- Ni muhimu kuwa msukumo wa kipekee katika utoaji.

Vifaa

- Mwongozo wa mwnafunzi: Tafakari ya 5 (1 kwa kila kikundi kidogo)

Utangulizi

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

- Nini kinakuja akilini mwako tunapoongelea kuhusu utoaji na zaka?
- Kitu gani kinakusukuma kutoa kwa wengine? Au Kanisani kwako?
- Je, dhana ya kibiblia ya kutoa ni nini?

Je, tunamwibia Mungu?

KIKUNDI KIDOGO CHA MJADALA

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Wagawe washiriki katika makundi ya watu 3-4. Gawa* ***Mwongozo wa Mwanafunzi****: Tafakari ya 5.*

SomaMalaki 3:8-12.

- Je, Wana wa Israeli walimwibia Mungu kwa namna gani?
- Je, ni yapi matokeo ya kumwibia Mungu?
- Je, Mungu anasema nini ikiwa tutaleta zaka kamili?
- Je zaka kamili ni nini?
- Je, huwa nasi tunamwibia yesuYesu?

Hizi ndozo aya pekee katika Biblia ambazo Mungu amesema kuhusu kumjaribu Anatumia lugha yenye uzito kuelezea taifa la Israeli hasa jinsi anavyojisikia kuhusu utoaji na zaka. Hukumu yao katika uasi wa kutokutoa zaka kuliwapelekea kuishi katika hali ya umaskini wa kutosha.

Utoaji toshelevu katika hali ya umaskini

KIKUNDI KIDOGO CHA MJADALA

Soma 2 Wakorintho 8:1-4

- Je, wakristo Kanisa la Makedonia walikuwa matajiri au maskini?
- Je, walitoa kiasi gani?
- Je, msukumo wao katika utoaji ulikuwa ni upi?
- Tunajifunza nini kutoka kwa Kanisa hili?

Kanisa la Makedonia walilkuwa ni maskini sana. Sisi si maskini sana. Ingawa tunaiona hali yetu na kudhani tuko hatika hali ya maskini sana, lakini kiuhalisia sivyo. Watu wa Makedonia bado walimtolea Mungu zaidi na zaidi ya walivyoweza. Hii ni changamoto kubwa sana kwetu! Mara kwa mara tunamtolea Mungu kutokakana na kile kinachosalia kwetu. Watu wale walimfurahisa sana Paulo kutokana na bidii yao katika utoaji. Je, tunamsukumo huo mioyoni mwetu? Je, tuna msukuo huo ndani mwetu wa kumtolea Mungu au tumekata tamaa?

Ubadhilifu kwa Mwanamke Mjane

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Soma Marko 12:41-44.

- Je, mjane huyo alitoa kiasi gani?
- Je, alikuwa Tajiri au Maskini?
- Je, mwitikio wa Yesu ulikuwa ni upi?

Wakati mwingine tunadhani kuwa tu maskini na hivyo hatuhitaji kutoa. Hii si kweli. Yesu hakumzuia mwanamke huyo kutoa. Wala hakusema "Wewe ni maskini mno, hebu tunza hiyo iwe akiba yako" Badala yake, Yesu alimsifu kwa utoaji wake.

Kutoa kwa Ukarimu na kwa moyo Mkunjufu

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Soma 2 Wakorintho 9:6-7.

- Je, ni kwa jinsi gani tunapaswa kutoa?
- Inamaana gani "Apandaye haba atavuna haba, apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu"?

Mungu ametuagiza kutoa. Haijalishi tunaishi katika hali ya umaskini au utajiri. Tunapaswa kutoa. Wote tunapaswa kutoa. Ikiwa hatutoi kama tulivyoagizwa, basi tunamwibia Mungu. Lakini, Kadri tutakavyotoa, ndivyo tutakavyozipokea baraka za Mungu. Mungu hutupatia baraka zake kwa kipimo sawa na kile tunachomtolea. Baraka tutakazozipokea kwake, zaweza kuwa ni fedha lakini pia Mungu anaweza kutubariki kwa kutupatia furaha, Amani, uvumilivu, familia yenye amani au kujiwekea hazina mbinguni.

- Je, nisababu gani inatusukuma kumtolea Mungu?

Yunapaswa kuwa waangalifu kwa kutoa tukitarajia kurudishiwa kitu. Hii siyo njia nzuri ya kutoa-ni kama kumkopesha mtu fulani fedha. Mungu hapendi sisi tumkopeshe fedha. Ni juu yake kuturudishia au la. Watu wengi wamefanywa wajinga kawa kufikiri kuwa wakitoa vitu vingi kwa Mungu ndivyo watakavyopokea vingi. Mungu huiangalia mioyo yetu; Yeye anajua mawazo yetu yote. Yeye pia anaweza kutubariki sisi kwa njia mbalimbali na kwa nyakati tofauti. Msukumo wetu katika kutoa daima unapaswa kuwa ni kumrudishia shukrani Mungu wa yote aliyotupatia. Mungu anapenda sisi tutoe kwa ukarimu badala ya kutarajia kupata kitu kutoka kwake.

PAMOJA NA MWENZI

Jadili mafunzisho haya ukiwa na mwenzako. Fikiria:

- Je, unamtolea Mungu kama unavyopaswa? Kwa nini?
- Je, baada ya kupata mafundisho haya, utachukua hatua ipi ya mabadiliko juu ya utoaji na zaka?

Kila mmoja wenu aombe kwaajili ya mwenzake. Ombea mitazamo mibayaa iliyoathiri mtazamo wako juu ya mtazamo sahihi katika utoaji.

Sehemu :2: Masomo Muhimu

Somo la 1: Utangulizi katika Bajeti

Mawazo Makuu

- Ni jambo la msingi kuwa na utaratibu mzuri juu ya fedha zetu

Vifaa

- Kielelezo: Bango kuhusu Gharama (1)
- Kielelezo: Mchezo wa Karata kuhusubajeti na deni– Kulingana na maelekezo ya uchapaji.
- Kielelezo: Picha ya nyumba tupu (1)
- Mwongozo wa Mwanafunzi: Mchezo wa mpanga bajeti
- Kifaa cha kukatia
- Weka karatasi na kalamu ili kuandika jumla kwa kila mtu au kikundi

Utangulizi

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

- Unadhani kuwa familia nyingi katika jamii hii zinachagua ni wapi na lini mahali pa kutumia fedha zao?
- Je, hali hiyo inaleta athari gani kwa jamii hiyo?

Mchezo wa Karata kuhusu Bajeti na Deni- Mwaka Mmoja

KIKUDI KIKUBWA CHA MCHEZO

Leo tutacheza mchezo wa matumizi ya fedha, na jinsi tunavyoweza kuweka mpango kuhusu kutumia fedha zetu.

Maelekezo ya mwezeshaji: *Waambie wajigwawe katika vikundi sita. Kuna vifaa vyakutosha kawa makundi yote sita. Chezeni kufuatana na maelekezo ya Muhtsari.*

Tutaanza na fedha kama kikindi chenu kitakuwa kimevuna mazao na muzitumie kadri mnavyohitaji. Kwa mwaka wote mtakuwa mmekutana na gharama zifuatazo.

*Bandika Bango lenye gharama – **Kielelezo**.Eleza safu ya gharama za zisizopangiliwa ueleze jinsi inavyofanya kazi.*

Gharama zisizopangiliwa ni zile tunazokutana nazo kila mwezi bila kutarajia kv. dawa, harusi, vifo. Ni vizuri kutambua ni kiasi gani utalipia gharama hizo, utatumia kete na kulipa mara 25,000 kulingana na namba zilizopo kwenye kete. Katika maisha unapaswa pia kufikiri kuhusu kuwekeza na utoaji/zaka. Haya yote ni muhimu sana lakini kwa wakati huu, havijawekwa kwatika mchezo wetu.

Kwa kuanza, umekuwa na mwaka mzuri kwa kilimo, na kuuza mazao kwa dola 6,250,000 Tsh. Kiasi hicho ndicho kipato ulichojipatia kwa mwaka huu. Ingwa mchele ulikuwa nao, basi kiasi hicho kilitosha kwa ajili ya chakula kwa miezi 9. Kwa hiyo utatakiwa kununua mchele mwingine wa ziada kwaajili ya miezi 3 mingine.

Gawa kwa kila kikundi 6,250,000 Tsh. (1,000,000–3; 500,000–5; 100,000–7; 10,000–3; 5,000–3, 500–10)

Leo umeenda dukani kufanya manunuzi ya vitu mbalimbali.

*Waonyeshe picha ya nyumba tupu – **Kielelezo***

Kama unavyoiona nyumba yako iko tupu; kwa kawaida una – mkeka, vyngu vichache, surufia chache na nguo za kawaida. Paa lako chakavu.

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Waonyeshe vitu vinavyotakiwa kuuzwa (karata zlizoandaliwa kutokana na* ***kielelzo****) kisha uulize ni nani anapenda kununua nini. Waruhusu wao kununua kile wanachotaka kununua. Kama kila mtu akimaliza kufanya manunuzi ya vitu ufafanue kwamba soko limefunguliwa kwa mwaka mzima, na wakati wowote kununua kitu chochote uakachohitaji.*

Ili kucheza mchezo huu vizuri, ni vizuri kufanya mahesabu ya gharama zako kawaida kwa mwezi. Hiki ndcho kiwango unachopaswa kulipa kila mwezi bila kuweka gharama zingine ambazo haziko kwenye mpango. Kama unavyoona kila mwezi unapaswa kulipa 75,000 Tsh. 5,000 kwaajili ya chakula, 12,500 Tsh. kwaajili ya umeme, na 25,000 Tsh. kwaajili ya wasambazaji wa kifamilia. Jumala yake ni dola 187,500 Tsh.

Kwa mkuongezea, unahitaji kulipa deni lolote mililokopa mwa mwezi.
Hii ndiyo jumla ya gharama utakazolipa kwa kila mwezi bila kuweka gharama za mahitaji yasiyo na mpangilio.

Kila kikundi kifanye mahesabu ya gharama za 'kawaida' za kila mwezi. Andika gharama za kila kikundi na uweke mbele ya kila kundi ili iwe rahisi kwao kukumbuka.

Sasa tutaanza mwaka wetu bila salio lolote.

Cheza kwa mwaka mmoja kama ifuatavyo (Meza yenye ufupisho unayoiona kwenya ukrasa ufuatao):

1. *Kikundi cha kwanza kifanye igizo kwa kete na kisha kuchukua gharama zao za kawaida + gharama zisizowekwa kwenye mpangilio.*
2. *Fanya hivyo kwa kila kikundi.*
3. *Fafanua kwamba, huu ulikuwa ni mwezi Januari. Endelea kufanya hivyo kama salio la mwaka ukitumia kila amzunguko kama ulivyo mwezi kama ifuatavyo:*
    - ***a.*** *Kila mwezi Feburuari wanajua kuwa wanapaswa kulipa kar ya shule 200,000 Tsh. kwa kila mtoto mmoja. Hivyo kila mtu anapaswa kulipia gharama za kawaida+ 400,000 Tsh. kwaajili ya kazoo +gharama ambazo hazina mpangilio kamili. Ikiwa yeyote atapenda kumtoa mtoto wake shuleni, anaruhusiwa*
    - ***b.*** *Mwezi Machi n Aprili ni sawa na mwezi Januari.*
    - ***c.*** *Katika mwezi Mei watoto wataanza mapema mwaka mpya wa masomo yao. Wanapatakiwa kulipia karo za shule, Sare, pmoja na vitabu. Lakini pia wanatkiwa kulipia 250,000 Tsh. kama ziada kwa kila mtoto.*
    - ***d.*** *Mwezi Juniwanatkiwa kununua mbolea na mbegu, hivyo kila kundi linatkiwa kulipa ziada ya 750,000 Tsh. kama kawaida pamoja na gharama zisizopangiliwa.*
    - ***e.*** *Miezi ya Julai, Augostina Septembainafanana na mwezi Januari.*
    - ***f.*** *Katik mwezi Oktoba, Novemba na Desembahutakuwa tena na mchele katika hala lako. Unatakiwa kununua mchele wa ziada kila mwezi kwa gharama ya 75,000 Tsh. kwa mwezi.*

Kama mtu Fulani akiingia katika deni, pitia maelekezoyanayohusu deni kam ilivyoonyeshwa hapa chini.

Maelekezo kuhusu Deni:

Kama hutaweza kulipia gharama za kila mwezi, unamachaguo mawili. Labda kuuza mavuno ya mwaka ujao kwa 5,250,000 Tsh.; au nenda ukachukue mkopo.

Fanua kuwa, mara kwa mara kuna riba nyingi ya kulipia mkopo. Itagharimu fedha inayoitwa gharama za deni. Hivyo basi, makusudi ya mchezo huu, haitakuwa kuhesabu riba kwa kila mwezi; bali ni kwa mwezi wa unaotanza peke yake.

Ikiwa watachangua kuuza mavuno yao mapema, basi wapatie t,250,000 Tsh.

Ikiwa watahitaki kukopa, basi wapatie Karata ya mkopo. Juu ya karata hiyo, andika kiasi cha mkopo (ukijumlisha 10%) na idadi ya miezi iliyosalia. Kwa mfano, ikiwa watakopa mwez Agosti na baada ya miezi 5(yaani kuanzia mwezi Agosti hadi mwezi Desemba).

Mpangilio wa Mchezo	
Januari	= gharama za kawida + Gharama zisizo na mpangilio.
Februari	= gharama za kawida + Gharama zisizo na mpangilio + 400,000
Machi	= gharama za kawida + Gharama zisizo na mpangilio
Aprili	= gharama za kawida + Gharama zisizo na mpangilio
Mei	= gharama za kawida + Gharama zisizo na mpangilio + 500,000
Juni	= gharama za kawida + Gharama zisizo na mpangilio + 750,000
Julai	= gharama za kawida + Gharama zisizo na mpangilio
Agosti	= gharama za kawida + Gharama zisizo na mpangilio
Septemba	= gharama za kawida + Gharama zisizo na mpangilio
Oktoba	= gharama za kawida + Gharama zisizo na mpangilio + 75,000
Novemba	= gharama za kawida + Gharama zisizo na mpangilio + 75,000
Desemba	= gharama za kawida + Gharama zisizo na mpangilio + 75,000

KIKUNDI KIKUBWA CHA TAFAKARI

Mnapofikia mwisho wa mchezo, Fanya mahesabu uone kama kuna mtu anadaiwa au hadaiwi.

- Kitu gani kilitokea katika mchezo huu?
- Je, kuna yeyote aliyeishia katika deni? Kwa nini umegundua hivyo?
- Mtu anajisikiaje anapokua katika deni?
- Je, kila mmoja anapanga jinsi ya kutumia fedha zake – hii imesaidiaje watu hao?
- Kitu gani chaweza kuwa tofauti kwa wakati ujao?

Kumbuka: Katika mchezo huu, kunafedha za kutosha kwa mtu kununua kila kitu anachohitaji pamoja na fedha zinazosalia!

Mchezo wa Kadi kuhusu Bajeti na Deni– Miaka Miwili

Wakati huu tunakwenda kucheza mchezo mwingine kwa mawaka mwingine, katika vikundi hivyo hivyo. Tutatumia idadi mfumo ule ule uliotumika mwaka wa kwanza ili kurahisisha; lakini kipindi hiki kama ukipenda utatumia mpangiliaji.

Fafanua yafuatayo– Usimamizi mzuri ulio na mafanikio kwa fedha zako ni pale unapoweka mpango kamili. kama utakavyoona kwamba, kila mwezi unapaswa kulipa kwa siku 30 x 5000 Tsh. kwaajili ya chakula, 12,500 Tsh. kwaajili ya umeme, na 25,000 Tsh. kwaajili ya mtumishi wa nyumbani.

Baadaye sasa tunatakiwa kuongeza gharama nyinginezo ambazo haziko kwenye mpangilio.

Hii ndiyo jumla ambayo ni 350,000 Tsh. (unaweza kuandika ubaoni au kwenye karatasi ngumu ili ionekane kwa wote) utafanya kama inayoonyeshwa kwenye mnyumbulisho uliopo hapa chini. Jumla kwa mwaka ni dola 350,000x12mezi =4,200,000 Tsh.

Gharama za mwezi

Kitu/Vitu	**Muda/mwezi**	**Gaharama kwa muda**	**Jumla ya gharama**
Chalula	30	5000	150,000

Umeme	1	12,500	12,500
Watumishi wa nyumbani	1	50,000	50,000
Gharama zisizopangiliwa	1	150,000	150,000
	Jumla ya zote gharama kwa mwezi		337,500
			X12
	JUMLA YA GHARAMA KWA MWEZI		4,050,000 Tsh.

Sasa tumepata gharama za Mwaka - ada ya shule, mchele wa ziada, na mbolea (ziongezwe kwenye karatasi kama inavyoonekana.) Hiyo ni jumala ya 1,875,000 Tsh. kwa mwaka.

Gharama za mwaka

Vitu	Idadi ya muda kwa mwaka	Gharama za muda	Jumala Kuu
Masomo – Februari	1	400,000	400,000
Masomo - Mei	1	500,000	500,000
Mchele wa akiba	3	75,000	225,000
Gharama za kipato	1	750,000	750,000
	JUMLA YA GHARAMA ZA KWA MWAKA		**1,875,000 Tsh.**

Sasa tumepata gharama zisizo na mpangilio. Hebu sasa tuweke bajeti kwaajili ya mwaka wa kutisha. Lakini kama tukigundua kuwa hatunahizo gharama zisizo pangiliwa, basi tunaweza kujikuta tunaziada ya fedha na hivyo tunaweza kuitumia kwa muda huo. (Tusitumie fedha kabla ya hatua hiyo). Hivyo, 6* 25,000 Tsh. ni 150,000 Tsh. kwa mwezi au 1,800,000 Tsh. kwa mwaka.

Kwa sasa tuna jumla ya 4,050,000 ambazo ni gharama za kila mwezi, 1,875,000 Tsh. kwa mwakanmzima. Jumla kuu ni 5,925,000 Tsh. Bila shaka tuna akiba ya 325,000 Tsh. Tunaweza kuchagua kuzitunza fedha hizi au kuzitumia. (Baadaye tutajifunza juu ya mpango mzuri wa matumizi ya fedha hizi.) Kila mwezi kama hutatumia fedha kwaajili ya gharama zisizopangiliwa, basi utakuwa na ziada.

KIPATO	**- GHARAMA ZA KWEZI**	**- GHARAMA ZA MAHITAJI KWA MWAKA**	**= SALIO**
6,250,000	**- 4,050,000**	**- 1,875,000**	**= 325,000 Tsh.**

Sasa katika makundi yenu, wekeni mpangilio wafedha zenu weye kufanana. Baadhi yenu mtajikuta na kipato kidogo kwa Sababu mliuza mashamba yenu mapema. Baadhi yenu mtajikuwa mna madeni yanayohitaji kulipwa. Hayo nayo mnapaswa kuyaunganisha.

*Gawanya **Mwongozo wa Mwanafunzi**: Mchezo unaohusu Mpanga Bajeti,1kwa kila kikundi.*

Kama watakuwa tayari, basi kila kundi uligawie 6,250,000 Tsh. kama nyongeza.

Ili kufanya kwa haraka zaidi, ni vizuri mtu mmoja aruhusiwe kutupa kete na kisha kila mmoja atakutana na baadhi ya gharama zisizopangiliwa.

Fuata maelekezo hayo ya mchezo kwa mwaka wote.

Kufikai mwishowa mchezo, fanya mahesabu ili kujua kila mmoja anadaiwa ninikatika kipindi hiki.

KIKUNDI KIKUBWA CHA TAFAKARI

- Je, kikundi chenu kina mpango wa kutumia 'Salio"? Eleza ni kwanini? Au kama si hivyo ni kwa nini?
- Je, ni mambo gani mengine uliyoyafanya katika mwaka wa pili tambayo ni ofauti na yale uliyofanya kwa mwaka wa kwanza?

  Toa mambo haya kama itakuwa vigumu kwao kueleza:
  - *Sio wakati wote ununue mahitaji Sokoni*
  - *Anza kwa kuhesabu gharama zinazohitajika na utenge kiasi hicho kabla ya kuanza manunuzi.*
  - *Ni vizuri kujua hilo mapema ingawa soko liko wazi wakati wote kwa mwaka mzima, bado tunaweza kuendelea kununua vitu vingine baadaye baada ya gharama zisizo na mpangilio kujulikana mapema.*
- Je, kuna utofauti upi kuhusu deni la kikundi chako kwa mwaka huu ukilinganisha na mwaka jana? Kiasi kikubwa? Kiasi kidogo?
- Unadhani kuna ugumu au urahisi upi kuweka mpango kwa mwaka ujao ili kuiepusha familia yako kuwa katika deni lolote? Kwa nini unadhani hilo ni jambo la msingi?
- Ikiwa utaweka mpango mapema, unadhani ni mambo yapi yatakuwa tofauti?

Katika masomo machache yafuatayo, tutaangalia swala zima la kuweka mpango kuhusu utumiaji wa fedha zetu.

Somo la 2: Kuandaa bajeti ya Kifamilia (Sehemu ya 1)

Mawazo makuu

- Tunafanya bajeti ili kupangilia jinsi ya kutumia vizuri fedha tulizopewa na Mungu.
- Hatu aya kwanza katika kutengeneza bajeti a kifamilia ni kufanya hesabu za kipato chetu halisi (inayobaki baada ya makato yote)
- Tunapaswa kutofautisha kati ya Matakwa na mahitaji

Vifaa

- Kielelezo: Bango lenye Bajeti: Hatua Nne za Bajeti (1)
- Kielelezo: Picha ya Karata za Mahitaji na Matakwa (1 seti)
- Mwongozao wa Mwanafunzi: Kuunda Bajeti Hatua ya 1
- Mwongozo wa Mwanafunzi: Kumbukumbu za matumizi ya Kifamilia
- Ubao na Kalamu kwaajili ya kuchora mifano
- Kadi tupu

Utangulizi

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

- Tunapopata fedha, huwa tunazifanyia kazia gani?
- Je, kuna miezi tunapata fedha nyingi na miezi mingine tunapata fedha kidogo?
- Je, tutahakikishaje kuwa tunaingiza fedha za kutosha kwa mwaka mzima?
- Je, tutafanya nini ikiwa hatuna fedha za kutosha? Je, kuna matokeo gani?
- Je, kuna wakati huwa unakoswa mahitaji ya muhimu?
- Je, unadahani unatumia fedha zako kulingana na Mungu alivyozikusdia zitumike?

Moja ya tatizo linalotukabili ni kwamaba, mara tunapozipata fedha tunazitumia zaidi, lakini zinapomalizika, kutunakuwa na njaa kubwa inayopelekea sisi kukopa. Ninaamini tunazikumbuka familia ambazo wakati wa mavuno ya mpunga wanakula vingi lakini kabla ya mavuno wananunua mchele zaidi kwa sababu hawana mchele wa ziada.

Tatizo jingine ni kwamba, mara kwa mara tumeshindwa kuandaa fedha kwaajili ya mahitaji muhimu kama vile shule, badala yake tunaamua kutumia vibaya dedha zetu. kwa mfano, tunatumia fedha nyingi ununua nguo kwa gharama kubwa baada ya mavuno na baadaye tunateseka. Hii siyo njia nzuri inayotufanya sisi tuitwe mawakili wema wenye kusimamia fedha za Mungu.

Bajeti

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Toa **Kielelezo** – Weka Bango lenye bajeti mahari ambapo kila mtu anaweza kuona.*

Ni sawa tu na mchezo tuliocheza awali, bajeti ni mapango unaohusu jinsi utakavyotumia fedha zako. Makusundi ya bajeti ni kuhakikisha unatumia kwa hekima fedha alizo kupatia Mungu, ili uweze kutunza familia yako kwa mawaka mzima. Kuna hatua Nne za msingi tutakazozipitia katika mchakato wa kuandaa bajeti.

1. Fanya hesabu ya kipato chako halisi (baada ya makato yote)
2. Fanya hesabu za mahitaji ya kipato chako chote
3. Fanya hesabu ili kujua tofauti
4. Tumia salio lako kwa hekima

Leo tutaangalia juu ya kuhesabu kipato chako halisi

A: Fanya hesabu ya kipato chako chote

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Melekezo kwa mwezeshaji: *Gawanya* ***Mwongozo wa Mwanafunzi*** *– Kuunda bajeti:* ***Hatua ya 1****.*

Hatua ya kwaza ni kutambua kiasi tunachopokea kwa mwaka. Kama una kazi ya yenye kukupatia mshahara, hatua hii haitakuwa ngumu kwako.Lakini kama wewe ni mkulima au mfanya biashara ndogondogo basi itakuwa ni vigumu kutambua hatua hii. Tutachunguza kwa undani zaidi jinsi ya kuhesabu kipato kinachotokana na kilimo na na biashara baadaye. Kwasasa, unaweza kukukisia kulingana na uwezo wako tu.

- Je, kuna chanzo gani cha mapato katika jamii yetu?
  - Mazao makuu – Mchele au nafaka; na mazao Mengine - mbogamboga
  - Ufugaji
  - Kazi za kila siku
  - Uuzaji/Uchuuzi
  - Kutoa huduma kv-Ufuaji nguo, Usafi na kulea watoto

KAZI KWA KILA MWANAKIKUNDI

Melekezo kwa mwezeshaji: *Chora Jedwali la 1 chini ya ubao. Hakikisha kila mtu anaelewa vizuri hilo Jedwali.*

Kipato	Muda kwa mwaka	Gharama kwa muda	Jumla
Zao la Mpunga	Aina 2za mazao kwa mwaka	2,500,000	5,000,000
Uuzaji wa vinywaji baridi	Chupa 500 kwa Mwaka	750	375,000
JUMLA YA KIPATO			5,375,000 Tsh.

Jedwali 1

Washirikia wanapaswa kukamilisha Jedwali la 1 lililomo katika Miongozo yao kulingana na kipato chao. Uwakumbushe kwamba kinachotafutwa hapo ni vitu vianavyotuingizia fedha. Kwa mfano: Hatutazingatia vitu kama kuku au mayai ambavyo hatuviuzi ili kujipatia fedha, lakini badala yake ni vile tunavyotumia kwa chakula. Na kama tukiuza mayai ili tujipatie fedha, basi inabidi tuviweke kwenye orodha ya vile vinavyotuingizia kipato.

Kumbuka pia, unahitaji kuorodhesha njia zote zinazokuingizia fedha. Kwa mafano labada unavuna nafaka na mpunga, unafanaya kazi za kila siku, na au unafuga nguruwe, au unaweza kuuza vinywaji laini, au kule watoto kwaajili ya kujiingizia kipato. Jaribu kuhesabu kiasi unachoingiza kutokana na vyanzo hivyo kila kimoja. Hesabu kila ulichojiingizia mwka uliopita. Andika jumla ya kipato chote na wala siyo mtaji tu.

Kumbuka kuweka kiasi utakachopokea kwa miezi 12 inayokuja. Hakikisha kwamba kama una mpango wa kufuga nguruwe, kuwauza, na kuzalisha zaidi, basi ufanye mahesabu kujua kiasi utakachouza kwa maka utakaofuata.

MSHIRIKISHE MWENZAKO

- Je, ukusudia kupokea kiasi cha fedha sawa na kile ulichopokea mwaka jana? Zaidi? au Pungufu?
- Kama ni zaidi, kwa nini? Je ni mabadiliko yapi yamesababisha uzalishaji zaidi?
- Kama ni pungufu, ni mabadiliko yapi yamesababisha wewe kupata hivyo?

B:Fanya hesabu za matumizi ya kipato chako

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Hatua inayofuata, tunahitaji kuongezea gharama za kipato chako. Hapa unapaswa kukadiria katika kila kundi lililochanganuliwa katika jedwali la 1, ili uweze kuona ni gharama zipi umetumia ili kufanihisha kazi hiyo.Tutaendelea kuangalia jambo hilo kwa undani baadaye tena, lakini kwa sasa tutatumia njia ya kukadiria.Kumbuka kuweka gharama zote za mwaka, wala siyo mradi mmoja tu.

Maelekezo kwa Mwezeshaji: *Chora mfano ubaoni kisha majadiliano yafanyike katika kikundi.*

Gharama	Mwaka mmoja	Gharama	Jumla
Zao la Mpunga	Mazao 2kwa mwaka	500,000	1,000,000
Uuzaji wa Vinywaji baridi	Chupa 500 kwa mwaka	500	250,000
JUMLA YA GHARAMA ZA KIPATO			1,250,000 Tsh.

Jedwali 2

- Ni gharama zipi katika makadirio zaweza kuwekwa katika kilimo cha Mpunga?
  Je, kuna gharama zozote katika uuzaji wa vinywaji baridi?
  - Usafiri kwenda eneo lalao la kazi
  - Ununuzi wa Vinywaji baridi
  - Barafu
- Kuna utofauti upi kati ya Jedwali la 2 na Jedwali la 1?
  - Katika kundi linaloonyesha Kipato linafanana na kundi linaloonyesha matumizi.
  - Tarajia namba kuhusu muda kuwa zilezile.

ZOEZI LA MSHIRIKI MMOJA MMOJA

Melekezo ya Mwezeshaji: *Hakikisha washiriki wamekamilisha jedwali la 2 lililomo kwenye Miongozo yao hasa kulingana na kipato chao. Wakumbushe kuweka gharma zote za mwaka mzima.*

C: Fanya hesabu ya kipato chako halisi

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Mwisho, sasa tutafanya mahesabu ju ya kipato chetu halisi.

Maelekezo ya mwezeshaji: *Chora mfano ubaoni kukamilisha sehemu hii. Onyesha utofauti kati ya jedwali la 1, 2 na la 3.*

JUMLA YA KIPATO	GHARAMA ZA KIPATO	KIPATO HALISI
5,375,000 Tsh.	- 1,250,000 Tsh.	=4,125,000 Tsh.

Jedwali 3

KAZI YA MTU MMOJA MMOJA

Sasa unaweza kukamilisha Jedwali la 3. Tambua Kipato chako kamili, toa gharama za kipato, kisha utapata kipato halisi.

Tambua gharama binafsi

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA *(Tumia kielelezo: Kadi zinazohusu Mahitaji na matakwa)*

Hatua ya pili katika kuunda bajeti ni kuzitambua gharama zetu. Ni jambo la msingi kutambua tofauti kati ya kitu tunachohitaji na kitu tunachotaka.

Maelekezo ya mwezeshaji: *Uliza kikundi kufikiria mambo mengi tofauti ambayo hutufanya sisi kutumia fedha zetu nyingi. Kama una Kadi yenye kitu kinachotajwa kiweke mbele yenu. Kama huna, basi chora au andika wazo hilo kwenye karata iliyo wazi. Kumbuka kuzingatia maeneo yafuatayo.*

- Ni baadha ya vitu gani hutufanya tutumie fedha nyingi?
    - Chakula
    - Huduma za nyumbani kv Maji, Gesi na Umeme
    - Gharama za matibabu
    - Elimu – Sare za shule, vitabu, na gharama zingine zinazohusu mambo ya shule.
    - Nguo
    - Gharama za usafiri, Mfano, Petroli, Matengenezo ya gari, Teksi, Mabasi, Magari Mengine.
    - Gharama za kipato – Fedha unayohitaji kutumia ili kuongeza kipato chako.
    - Zaka

Mara watakapomaliza, kama bado utakuwa na karatai zenye picha uwaulize kitu kilichopo kwenye kadi kitakuwa miongoni mwa vitu vinavyowafanya watumie fedha nyingi kununua.

Uliza kikudi kugawanya kadi katika makundi mawili-'Mahitaji' na 'Matakwa'."Mahitaji" ni mambo ambayo lazima tuwe nayo ili tuweze kuishi au kupata mapato au kutoa mahitaji ya kiwango cha chini kwa familia zao. "Matakwa" ni mambo ambayo tungependa kuwa nayo.

Waruhusu kugawanya kadi katika makundi mawili na kisha jadili kuhusu maamuzi watakayoyachukua kuhusu karata hizo. Hakikisha kadi zilizowekwa kwenye kundi la "mahitaji" ni muhimu kwaajili ya maisha yao — bila kuwa nayo basi watakufa. Hii ni pamoja na chakula, mbegu, elimu, nk "Matakwa" inapaswa kujumuisha mambo ambayo hufanya maisha yawe mazuri zaidi, lakini hatakama hayapo bado tunaweza kuishi, hata kama nyumba zetu hazina paa jipya.

Kadi za picha ziko hapa chini. Tafadhari Kumbuka kwamba, Mahitaji utatumia herufi (H) wakati Matakwa ukitumia herufu (T). Mapendekezo yako hapo chini.

Kulisha mfugo(H)	Mlo mzuri (T)	Ada ya shule (H)
Mlo wa kawaida(H)	Dawa(H)	Mbegu za kupanda(N)
Baiskeli(T)	Pikipiki(T)	Vifaa(H)
(H/T) Nguo	Gazeti(T)	TV (T)
Vinywaji baridi(T)	Kikaango kipya(T)	Sare(H)
Umeme, Feni (T)	Taa ya mafuta(H)	Vazi (W)
Friji(T)	Radio(T)	Maji(H)
Gesi(H/T)	Kitabucha shule (H)	

Ni jambo la msingi kujua tofauti iliyopo kati ya vitu tunavyotaka na vitu tunavyohitaji. Wakati tuanapokuwa tukitengeneza bajeti zetu tunapaswa kuweka kipaombele chetu kwenye vitu tunavyohitaji, na baadaye kama fedha imesalia tunaweza kununua vitu tunavyotaka.

Tunza kumbukumbu ya fedha zote zilizotumika

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Ili kutusaidia sisi tufanikiwa kuhesabu gharama za matumizi yetu, ambayo ndiyo njia pekee hatu aya kuandaa bajeti, ni kwa kutunza kumbukumbu zinazohusu matumizi ya fedha zetu. Jambo hili angalau linaweza kufanyika mara moja kwa mwezi au mara mbili kwa mwezi ili tuweze kupata picha kamili kuhusu matumizi ya fedha zetu. Ninaamini utashangazwa sana na matokeo. Muda mwigine, tunaweza kununua kitu flani kwa

gharama ya 5000 Tsh, lakini kwa kununua kila mara, mfano vitafunwa kwaajili ya watoto, mara kwa mara tunaweza kujikuta tumetumia fedha nyingi mno kwa muda wa mwaka mzima.

Kama tukitumia 2500 Tsh. mara tatu kwa wiki kununua chai, baadaye tutajikuta kwa mwaka tumetumia 390,000 Tsh.
Kama tukinunua pipi kwa 2500 Tsh. kwa siku, italeta jumla ya 912,500 Tsh. kwa mwaka.
Kama tukinunua kitu kama vile kahawa au sigara au beteri kwa 12,500 kwa siku, utajikuta kwa mwaka umetumia dola 4,562,500 Tsh.

Siyo kwamba kutunza kumbukumbu za matumizi ya fedha zetu hutusaidia kuunda bajeti, lakini pia inatusaidia kutambua maeneo ambayo tunaweza kupoteza fedha zetu pasipo kujua.

Hatua ya vitendo

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Gawanya* ***Mwongozo wa Mwanafunzi*** *– Kumbukumbu za gharama za Kifamilia*

Unaweza kutumia ukrasa huu kutunza kumbukumbu za kila kitu unachokinunua wewe pamoja na familia yako kwa wiki inayokuja na kuendelea.

Somo la 3: Kuandaa bajeti (Sehemu 2)

Mawazo Makuu

- Hatua ya pili katika kuandaa Bajeti ni kuhesabu mahitaji yetu binafsi kwa mwaka mzima.
- Baada ya hatua hii hesabu tofauti kati ya kipato chetu na mahitaji yetu.

Vifaa

- Kielelezo: Bango la bajeti (1)
- Mwongozo wa Mwanafunzi–Kuandaa Bajeti hatua ya 2 na 3 (Mmoja kwa kila Mshiriki)
- Karatasi kubwa au Ubao mkubwa kwaajili ya Chemsha bongo na mifano
- Kalamu

Utangulizi

KUKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Maelekezo ya Mwezeshaji: *Toa **Kielelezo**–Bango la bajeti mahali panapoonekana kwa kila mmoja ili liwe rejea unapoendelea na somo lako.*

- Je, utawezaje kutunza kumbukumbu za gharama zako?
- Je, kuna jambo lolote linalokushangaza?

Sasa tutakamilisha Hatua ya 2 na 3 kwaajili ya kuunda bajeti ya familia yetu.

Hatua ya 2: Fanya mahesabu ya mahitaji yako

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Baada ya kutunza kumbukumbu za gharama zetu kwa mwezi, sasa tunaweza kuandika bajeti yetu. Kama hatujafanya hatua hii, basi tunaweza kufanya makadirio tu. Tutaangalia juu ya mahitaji yetu kwanza.

- Je, nimahitaji yapi tuliyonayo sisi sote ili tuweze kuishi na kuzitunza familia zetu vizuri?

Maelekezo ya Mwezeshaji: *Adika matokeo kwenye Karatasi kubwa au ubaoni. Hakikisha kila kitu kilichopo kwenye orodha ni kile kinachohitajika na wala siyo kile ambacho tungependa kuwa nacho.*

Kulingana na mchezo uliochezwa hapo awali, unapaswa kukumbuka kuwa baadhi ya gharama zinapaswa kulipwa kila mwezi, wakati nyingine zikilipwa mwishoni mwa mwaka (Karo ya shule, gharama za matibabu, manunuzi ya mbegu.) Hebu fikiri juu ya maeneo yafuatayo:

- Chakula
- Huduma – Ni pamoja na maji, gesi, umeme
- Gharama za matibabu
- Elimu – Sare, vitabu na gharama nyingine za shule.
- Kuvaa
- Gharama za usafiri, mfano; petroli, Matengenezo ya gari, teksi, Basi, Magari mengine.
- Zaka

Sasa gawanya orodha hiyo katika makundi mawili tofauti:

- Gharama za kawaida za mwezi – Hivi ni vitu tunavyotakiwa kulipia kila mara.
- Gharama nyiniginezo – Hivi ni tutu tunvyolipia mara cache kwa mwaka.

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Chora mfano wa jedwali ubaoni kisha ufanye majadiliano na kikundi.*

GHARAMA ZA KAWAIDA ZA KILA MWEZI

Hitaji	Idadi ya muda kwa mwezi	Gharama	Jumla
Chakula	30	5000	150,000
Umeme	1	10,000	10,000
Maji	1	7,500	7.500
Zaka	4	7,500	30,000
Gharama za nyumbani: Mfano: Usafi, Vifaa	4	5000	20,000
Twisheni/Malipo ya ada ya Shule kwa kila mwezi	1	12,500	12,500
Usafiri	30	250	7,500
Gharama ndogo kwa Mwezi Mmoja			237,500
Hesabu 20% kwa mahitaji mengineyo			47,500
JUMLA MWEZI MMOJA			285,000
Zidisha mara 12 JUMLA YA MWAKA MZIMA			3,420,000

Kumbuka: Mwishoni mwa kila jedwali kuna asilimia ya ziada ya "Ziada."

- Je, unafikiri ni kwa nini tuongeze 10% au 20%?
    - *Ingawa tunajaribu kukisia gharama sahihi, tunaweza kujikuta tumesahau na kudharau gharama za ziada. Hizi ni gharama nyingine zisizotarajiwa kabisa. Ili kuhakikisha kwamba bajeti yetu ni ya kweli tunapaswa kuwa na nafasi kwa gharama zisizotarajiwa. Moja ya njia itakayotusaidia kufanya vizuri, ni kuongeza asilimia (kama 10%.) Njia nyingine ni kuongeza kiasi fulani, kama vile 25,000 Tsh. kwa mwezi. Hii hufanyika kwa kutenga fedha kidogo kwa ajili ya gharama zisizotarajiwa (ziada), n hapo tutakuwa na uhakika na kuendelea na bajeti yetu.* Kama fedha imesalia mwishoni mwa mwaka, basi unaweza kuongeza kwenye akiba yako au kuitumia juu ya kitu maalum.

GHARAMA ZA ZIADA

Hitaji	Idadi kwa Mwezi/mwaka	Gharama	Jumla
Sare za Shule	1	75,000	75,000 Tsh.
Vitabu vya Shule	1	37,500	37,500 Tsh.
Mavazi/Vitu	2	37,500	75,000 Tsh.
Ukarabati wa Nyumba	1	62,500	62,500 Tsh.
Jumla ndogo kwa Mwaka Mmoja			250,000 Tsh.
Hesabu asilimia 10% ya Gharama za zada			25,000 Tsh.
JUMLA KUU KWA MWAKA			**275,000 Tsh.**

ZOEZI BINAFSI

Maelekezo ya mwezeshaji: *Gawa* ***mwongozo wa mwanafunzi****: Kuunda bajeti hatua 2 na 3. Ikiwa wengi wa waliodarasani hawajui kusoma na kuandika, basi uwashauri wajigawe kwenye makundi ya watu wawili wawili au watatu watatu, uwaambie wasome kwa pamoja*. Wale wanaojua kusoma na kuandika wanaweza kuwaandikia wenzao.

Kwakutumia orodha ya mahitaji tuliyoifanya, sasa kamilisha "Jedwali la Gharama za kawaida" (Jedwali 4) na "Jedwali la gharama za ziada" (Jedwali 5) katika kitini, kwaajili ya familia yako.

Kumbuka aina zote za gharama za kila mwezi. Kama kuna kitu chochote hujakiweka basi ukiongeze kwenye orodha katika jedwali.

Mara baada ya kukamilisha, shirikisha mpango wako kwa wengine na uwaulize maana kw kufanya hivyo wanaweza kukumbusha ikiwa kunakitu umekisahau.

Hatua ya 3. Fanya hesabu ili kujua tofauti iliyopo

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Hagua hii imeusaidia kujua kipato chetu kwa mwaka na mahitaji yetu ili tuweze kuishi. Sasa ni wakati wa kuhesabu ili kupata tofauti iliyopo ambayo ndiyo hatua ya 3 ya Bajeti.

Kwa mfano:

Kipato halisi	**- Gharama za kawaida**	**- Gharama nyinginezo**	**= JUMLA**
4,125,000 Tsh.	-3,420,000 Tsh.	-275,000 Tsh.	=430,000 Tsh.

Katika kitini chako hebu sasa toa kiasi cha gharama hizo mbili kutoka kwenye KIPATO HALISI ukitumia Jedwali la 6.

- Je, umepata salio hasi au chanya?

Salio hasi

Ikiwa kipato chako kiko CHINI kuliko matumizi yako, basi salio utakalolipata lazima litakuwa ni Hasi. Hii inamaanisha kwamba utajikuta umetumia zaidi ya kipato chako, na hilo ni tatizo. Hakikisha mahitaji unayoyaorodhesha, ni “mahitaji kweli”. Je, ni kweli kuna kitu kati ya hivyo ulivyoviorodhesha ambacho huna kabisa? Je, kuna kitu ambacho ungependa kukitoa kisiwekwe kwenye orodha ya mwaka huu?

Ikiwa hakuna kitu ambacho unaweza kutoa sadaka na wakati huo salio lako liko hasi, basi unapaswa kufikiria jinsi ya kuwa na chanzo kingine cha mapato ili kukidhi mahitaji yako yote. Deni liapaswa kuchukuliwa katika hali ya dharura, au kwa ajili ya gharama ya kuzalisha mapato tu.

Somo la 4: Kujua jinsi ya kutumia fedha vizuri

Mawazo makuu

- Ziko njia nyingi za kutumia fedha
- Kuweka akiba ni njia nzuri mno kwa Sababu hutusaidia zinapotokea ghrama za dharula
- Uwekezaji ni njia nzuri sana maana hutusaidia kuwa na na fedha nyingi siku za mbele.
- Utoaji ni muhimu sana kwa Sababu tunaonesha jinsi tunavyomheshimu Mungu na kwa kumtukuza Yeye.

VIFAA

- Kielelezo: Njia za kutumia pesa-"kula", "kutunza", "kuwekeza" na "kutoa" (1 nakala)
- Kielelezo: Mchezo wa kadi unaohusu Mtu tajiri na mtu maskini (na maharagwe kwa pesa kama unayopendelea)
- Mwongozo wa mwanafunzi: mtu tajiri, sheria ya mchezo mbaya wa mtu maskini (1 kwa mshiriki)
- Kadi tupu (20 kwa kikundi kidogo)
- Alama (1 kwa kikundi kidogo)

Utangulizi

KIKUNDA KIKUBWA CHA MAJADILIANO

- Ni mambo gani unayoweza kuyafanya kwa kutumia fedha?

Kula, Kutunza, Kuwekeza, Kutoa

KAZI ZA VIKUNDI VIDOGO

Maelezo ya Mwezeshaji:*Gawa washiriki katika makundi 3.Wape kadi 20 kila kikundi na waambie waandike wazo moja katika kila kadi ambalo wanaweza kufanya kwa kutumia pesa Waambie wafikirie mambo mengi kama vile "kununua chakula,""kununua nguo," "kuweka akiba," "kununua ardhi," "kununua ngombe," "kununua bidhaa za kuuza," "kuwapa maskini," (unaweza usiandike chochote "kununua mchele," "kununua karoti," "kununua nyanya," "kununua nguruwe"…).Watunze kadi hizo kusubiri mjadala wa kikundi kikubwa, utakaofuatia.*

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA – Vielelezo: Njia za kutumia fedha

Kuna njia nne za kutumia fedha.

Kwa Mfano, Mkulima wa mahindi anapokuwa amevuna mahindi, kuna mambo manne anayoweza kuyafanya.

1. "**Kula**" – kuyatumia yote kwa chakula, hayatakuwepo tena kwa matumizi baadaye na hayatasaidia kuleta kipato cha pesa baadae.
2. "**Kutunza**" – Kutunza kwa ajili ya chakula cha baadae. Hii ni pale tunapotenga au kutunza pesa kwa ajili ya baadae – inakuwepo kwa ajili ya matumizi ya wakati mwingine.
3. "**Kuwekeza**" –Kutunza mbegu kwa ajili ya mwaka ujao. Hii ni pale tunapotumia pesa inatusaidia kukusanya nyingi zaidi baadae.
4. **"Kutoa"** – Kutoa mahindi kwa wengine. Hii ni vile tunapotoa pesa, yawezekana kwa mtu yeyote au kutoa kanisani kama zaka.

Maelezo ya Mwezeshaji: *Weka alama zote (Kula, Kutunza, Kuwekeza, Kutoa) juu kwenye sakafu. Waambie waziweke kadi walizoziandika juu ya alama ulizoziweka.Hakikisha wameweka kadi sehemu sahihi ya alama na kwamba wameelewa vizuri.Baada ya hapo,toa ufafanuzi:*

Endapo tutakula kitu chochote, hakika kitakuwa kimetoweka—hatutakuwa nacho tena baadae.

Endapo tutatunza kitu, tutakitunza kwa ajili ya baadae ili tukitumie kwa kula kwa wakati mwingine.
Endapo tutawekeza kitu, tutatumia pesa kwa njia ambayo zitaongezeka ili kwamba tuwe na pesa nyingi kipindi kijacho.

Endapo tutatoa kitu, tutawapatia wengine kuonyesha utii wetu kwa Mungu.

- Mifano gani ya kuonyesha namna ya kutunza pesa?

Maelezo ya Mwezeshaji: *Waambie washiriki waongeze tena mawazo 5 ya namna ya kuwekeza pesa.*

Mchezo Mtu tajiri, Mtu maskini

MCHEZO KIKUNDI KIKUBWA –*Tumia **Mwongozo wa Mwanafunzi**: Mtu Tajiri, Mtu Maskini kanuni za Mchezo; Vielelzo: Mtu Tajiri, Mtu Maskini Kadi za Mchezo.*

Ili kutusaidia kuelewa vizuri wazo hili na matokeo tutacheza mchezo.

Maelezo ya Mwezeshaji: *kugawa washiriki katika makundi ya watu 2 -3 Ikiwa watakuwa punguya watu 8, wanaweza kucheza binafsi. Gawanya kanuni za mchezo, **Mwongozo wa Mwanafunzi** .Rejea kanuni za Mchezo.*

1. Gawanya kadi 10 za pesa (au mahindi) yenye thamani sawa kwa kila kikundi.
2. Wape muda mfupi kufikiri na kuamua jinsi ya kutumia pesa zao.
3. Pita kwa kila kikundi uchukue kadi za pesa kwa jinsi walivyochagua kuishi, fanya yafuatayo:
    a. Wapatie vikundi kadi zao za mahitaji ya nyumbani na/ au kadi ya kuwekeza ikiwa walinunua moja.
    b. Gawanya kadi 6 za afya na kadi za afya na kadi moja ya ugonjwa, na kisha waambie wao wachague kadi.
    c. Ikiwa amepata kadi ya ugonjwa, itawalazimu kulipia kadi 2 zaidi za pesa. Ikiwa hawataweza kulipa mapema itawalazimu kupoteza kadi3 kutoka katika pato lao jingine.
4. Kama kila kikundi kimekamilisha zoewzi hiilo, basi unaweza kutoa kadi 10 za pesa kwa ajili ya hatua inayofuata, ukiongeza pesa ya kadi za ziada kulingana na jinsi ulivyowekeza au kutimiza mafunzo. Ondoa kadi 3kwa yeyote aliyepata kadi ya ugonjwa wala hakuweza kulipa mapema.

Cheza mara nyingine tena. Cheza kwa awamu nyingine chache.

Uwakumbushe vikundi kuhusu kuwekeza ikiwa hakuna ambaye amewekeza.

Baada ya mzunguko mwingine ikiwa wametumia pesa katika mchezo, hebu uwasaidie kufikiri faida zitakazopatikan ikiwa wametumia fedha zao badala ya kuwekeza.

Cheza tena mizunguko michache watu wakiwa wametunza na kuwekeza.

KIKUNDI KIKUBWA CHA TAFAKARI

- Kitu gani kilitokea katika mchezo huu?
- Ulijisikiaje wakati unacheza mchezo huu?
- Ulifanyaje uamuzi ili kufanya kitu?
- Je ulikuwa na fedha ya kutosha wakati wote ulipotaka kufanya kitu chochote?
- Ni kwa namna gani mchezo huu unahusiana na ukweli?
- Maskini wanapokuwa na pesa ya ziada mara nyingi wanazitumiaje?
- Kwa nini ni vigumu kwa maskini kuwekeza?
- Kwa nini unafikiri kwamba ni muhimu kwa maskini kuwekeza?
- Kitu gani kirahisi kifanyike ili mtu maskini aweze kuwekeza?

Inawezekana kwa maskini kutunza au kuwekeza? Majumuisho:

- Ni vigumu kwa maskini kuwekeza na kutunza, lakini wakiwa na nia wanaweza kujitoa na kuboresha maisha yao.
- Mojawapo ya mtego mkubwa kwa maskini ni kujikuta katika uhitaji wa kifedha. Ili kuzuia hilo kutokea maskini anapaswa kujiandaa kifedha ili kukabiliana na matukio makubwa ya kimaisha kama vile sherehe ya arusi,mazishi,ugonjwa n.k
- Mara nyingi maskini wanapopata pesa wananunua vitu kama vile Video au chakula cha ziada. Ingawa hakuna ubaya kwa vitu hivyo,siyo chaguo bora. Ikiwa maskini watawekeza itawezekana kuboresha maisha yao muda mwingi.
- Kitu kisicho kizuri kwenye mchezo huu, mara nyingi maskini hawatumii pesa zao kwa busara. Watu wengi maskini watakuambia hawana pesa ya kutunza ingawa wana kipato cha kutoshereza kununua pombe.

PAMOJA NA MWENZAKO

Jadili:

- Kiasi gani cha pesa ya familia yako unchokula, kutunza, kuwekeza, au kutoa?
- Je unafikiri ni kiwango sahihi? Unawekeza za kutosha? Unatunza za kutosha? Unatoa za kutosha?
- Unawezaje kuwekeza zaidi?

Mwongozo wa Mwanafunzi: Kanuni za Mchezo Mtu Tajiri Mtu Maskini

Kipato
Kila kikundi kilipokea kadi 10 za pesa (au maharage) kila mzunguko

Matumizi
Kila kikundi wataamua jinsi gani wanavyotaka kutumia pesa yao. Hupaswi kutumia kadi zote za pesa katika kila mzunguko.

- Chakula - Milo miwili kwa siku 5
  - Nyama 7
  - Kiwango cha Juu 10
- Umeme 2
- Shule kwa Watoto 1 kila mtoto (unao watoto 3)
- Vitu vya nyumbani
  - Latrine 5 Kochi Jipya 2
  - Baiskeli 2 Marekebisho ya Dari 5
  - Video 3 Stereo 1

Kadi ya Ugonjwa
Endapo unaumwa utatakiwa kulipa kadi 2 kwa ajili ya kutoa na madawa.Endapo hautakuwa tayari kulipa mapema hivyo utapoteza kadi 3 kutoka kipato kijacho.(mbili kwa ajili ya madawa na moja kwa ajili ya garama za pesa) (two for the medicine and one for money lender charges.)

Kuwekeza
Kila mzunguko unaweza kuchagua kuwekeza pesa. Unapowekeza lazima ziwe kadi 3 za pesa. Kwa kila kadi 3 za pesa ulizowekeza unapata ziada 1 ya kadi za pesa kwa kila mzunguko uliowekeza. Kwa muda wowote, unaweza kuuza uwekezaji wako lakini utapata kadi 2 za pesa kwa uwekezaji ambao umeuuza.

Shule/Ada
Kwa kilamtoto aliyekamilisha mizunguko mitatu ya shule utapewa ziada ya kadi 3 za pesa kwa kila mzunguko.

Somo la 5: Kupanga Bajeti ya Familia (Sehemu 3)

Mawazo Makuu

Kuna mambo matano ambayo yanawea kufanywa kwa kutumia pesa ambazo zimebaki baada ya kutoa mahitaji kwenye kipato halisi:

- Kutunza
- Kuwekeza
- Kutoa
- Utumiaji juu ya "Matakwa."
- Akiba maalumu

Vifaa

- Vielelezo: Bango la Bajeti (1)
- Vielelezo: Njia Tano za Kutumia Fedha
- Mwongozo wa Mwanafunzi: Bajeti Hatua ya 4 (1 kila mshiriki)
- Ubao/Karatasi Kubwa na Karamu
- Washiriki watahitaji nakala zilizokamilika za Hatua ya 1 – 3 ya bajeti, Chati 1 – 6.
    - Hizi zinazopatikana kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi 2.1, na Mwongozo wa Mwanafunzi 3.
- Mwezeshaji awe na nakala iliyokamilika ya Mifano katika Mwongozo wa Mwalimu Hatua ya 1 – 4; Jedwali 1 - 7

Utangulizi

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

***Maelezo ya Mwezeshaji: Weka kielelezo cha Somo la** 2: Bango la Bajeti mahali ambapo kila mmoja anaweza kuona ili kufanya marejeo wakati wa Somo.*

- Katika hii jamii, watu wanatumiaje pesa ya ziada ambayo wanaipata?

Hatutaangalia Hatua ya 4 ya Bajeti: Jinsi ya kuamua namna ya kutumia kile tulichobakiza, kwa busara.

Njia Tano za kutumia fedha

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Si kila mmoja atakuwa na baki la hasi anapokuwa na bajeti kutoka Hatua ya 1 mpaka Hatua ya 3. Ikiwa hautakuwa na baki la hasi hivo anza kuweka mipango ya jinsi utakavyotumia pesa ya ziada. Kuna mambo matano tofauti ambayo unaweza kuyafanya na baki la chanya.

***Maelekezo ya Mwezeshaji: Chora picha inayoonekana kwenye kielelezo cha Somo la** 5: Njia tano za kutumia pesa, moja kwa wakati, mkiwa mnajadili kila mada Husisha na mchezo uliochezwa nyuma kwenye somo lililopita kama linaendana.*

1. Kutunza

Kumbuka hadithi ya Yusufu kwenye Biblia?

- Kuna mmoja wetu anayependa kutusimulia sisi sote?

Yusufu aliuzwa utumwani na akapelekwa Misri. Baada ya kushitakiwa kwa uongo aliwekwa gerezani. Siku moja Farao akaota ndoto ambayo hakuielewa. Watu wake wote wenye hekima hawakuweza kumwambia maana ya ndoto.Ndipo myweshaji akakumbuka kwamba alipokuwa gerezani Yusufu alimtafsilia ndoto yake.Yusufu akapelekwa kwa Farao na kwa msaada wa Mungu akamwambia maana ya ndoto.Katika

ndoto kulikuwa na ngombe saba wanene na ngombe saba wembamba.Ngombe saba wembamba wakawala ngombe saba wanene waliokuja kwanza.Lakini baada ya kuwala wale hakuna ambaye angeweza kueleza kwamba wameliwa ngombe saba wanene.The same happened with the grain.Yusufu akaeleza kwamba hii ina maana kutakuwa na miaka saba ya mavuno na miaka saba ya njaa.Akamshauri Farao kutunza chakula katika miaka mizuri kwa ajili ya miaka mibaya. Farao akakubali ushauri wake na Misri ikaepushwa na njaa.

Kama ilivyokuwa wakati wa Yusufu, hata sisi pia tutakabiliana na wakati mzuri na wakati mbaya katika maisha yetu. Inaweza kuonekana kwamba wakati wote ni nyakati mbaya, lakini ikiwa tumebakiwa na kitu baada ya kufanya malipo ya muhimu, hivyo siyo wakati mbaya – ni wakati wa kutunza. Katika maisha yetu tutakabiliana na nyakati za aina zote wakati tunahitaji pesa – ugonjwa, crop failure, arusi na mazishi, n.k. Kama vile Mungu alivyomwonyesha Yusufu, tunahitaji kutunza wakati tunapokuwa na kitu cha ziada ili kwamba tujiandae kwa wakati mbaya. Ingawa tunatunza kiasi kidogo kwa muda, itaweza kutujenga. Ikiwa unahitaji kukopa kwa muda wakati kuna dharura hivyo utakabiliana na wakati mgumu wa kujitoa katika umaskini.

Ikiwa una kitu cha ziada, hivyo kitu cha kwanza cha kufanya ni kuweka kiasi pembeni kwa ajili ya garama za matibabu, n,k.

2. Kuwekeza

Njia nyingine ambayo tunaweza kutumia pesa zilizoachwa ni kuzitumia kwa kitu ambacho kitatusaidia kuingiza nyingi kipindi kijacho. Tunao uzoefu wa mchezo katika somo lililopita. Ikiwa tutawekeza pesa hivyo baadae itatusaidia sisi kuongeza pesa zaidi. Katika bajeti yetu tulishaweka na kutenga pesa kwa ajili ya kilimo mwaka ujao. Kuongezea ikiwa kuna pesa za kutosha itatupasa kuwekeza kidogo kwenye vyanzo vipya za mapato kama vile ufugaji (kuku, bata, mbuzi) bwawa la samaki, bustani ya mboga au miti ya matunda. Fikiria kwa makini kuhusu mambo mengine ambayo unaweza kufanya kukuza kipato chako. Endapo utaanza na shuguli mpya za kipato kidogo, hivyo mwaka ujao utakuwa na fungu la kuwekeza katika shughuli kubwa ya kipato. Utaanza kuondokana na umaskini ikiwa utawekeza pesa yako ili kwamba kila mwaka utaweza kuingiza zaidi ya mwaka uliopita.

- Ni njia zipi ambazo unazoweza kuwekeza pesa?

3. Kutoa

Biblia inatuambia kwamba Mungu atatupatia kutumia kipimo kile tunachotoa (Luka 6:38) Endapo tutakuwa waaminifu katka utoaji wetu, hivyo Mungu atakuwa mwaminifu katika kutubariki sisi, lakini endapo tutatoa kidogo, Mungu atazuia Baraka kwetu. Tunapaswa kuanza kwa kutoa zaka, lakini pia tuangalia watu wengine au miradi tunayoweza kuitolea.

- Kitu gani unachokitafuta zaidi? Nafasi ya kupokea zawadi au afasi ya kutoa zawadi?
- Ikiwa kweli tunaamini Luka 6:38, kipi kitakuwa kipaumbele? Kupokea au kutoa?

4. Kutumia katika 'Matakwa'

Hakika endapo kuna pesa ikiwepo hivyo tunaweza kuitumia vitu tunavyohitaji. Unahitaji kuangalia kwa makini katika orodha ya vitu unavyohitaji na kuamua kipi ni cha muhimu zaidi kwako. Hatupaswi kushawishika na kutaka kuwa kama familia zigine, lakini tufikilie kwanza kitu kinachomtukuza Mungu. Kukarabati nyumba au kujenga choo ni mambo mazuri. Ingawa tunatakiwa kuwa makini kuhusu kutumia zaidi pesa kwenye vitu kama vile Video na pikipiki labda kama pesa ipo. Kuliko kununua vitu ilimradi kujifurahisha au kulazimika, ni muhimu zaidi kuwekeza pesa ili kukuza kipato chako kwa mwaka ujao. Ikiwa kipato chako kinakuwa hivyo unaweza kutumia pesa kwa vitu kama hivyo. Sababu bajeti yetu inazingatia kiwango tunachotaka kwa kuishi pia tungetamani kuongeza posho zetu za mwezi kwa kiasi kidogo ili kurahisisha maisha ili kwamba tuweze kumudu kutoka na nje kwa ajili ya kahawa n.k.

5.Akiba maalumu

Mwanzoni tulitaja kutunza kwa tahadhari na kwa matumizi yasiyotarajiwa. "Akiba maalumu" maana ya kutunza ukilenga mradi maalum, kama vile kujenga nyumba mpya au kununua pikipiki. Vitu hivi vitahitaji muda zaidi ya mwaka kutunza pesa yake. Ni vizuri kuvumilia kutunza kwa ajili ya matumizikuliko kwenda kukopa ili ukavinunue. Unaweza kutunza na kutenga kiasi cha pesa kila mwaka kwa ajili ya matumizi haya. Njia nyingine ya kutunza kwa ajili ya hivi vitu ni kuwekeza katika vitu na ndipo unatumia faida kwa mradi maalum. Kwa mfano, unaweza kuweka katika miti sasa na inapokuwa tayari kuvunwa ndipo utakuwa na pesa za kuendeleza nyumba yako. Unapaswa kuwa mvumilivu na kusubiri mpaka upate pesa.

- Je ni matumizi gani makubwa ambayo ungependa kutunza kwa ajili yake?

Hatua ya 4: Tumia salio kwa hekima

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Tumeandaa Hatua 1,2 na 3 ya bajeti yetu. Sasa tunaweza kugundua jinsi tutakavyotumia salio lolote.

Katika somo 3 tulimaliza kutengeneza sehemu ya kwanza ya bajeti yetu. Tulikuwa na dola 172 iliyobaki. Sasa tutaanza kufanya mipango namna tutakavyoenda kufanya na hizo dola 172.

***Maelezo ya Mwezeshaji**: Chora mchoro ufuatao kwenye ubao au kwenye karatasi kubwa.*

Eneo la Bajeti	**Kiasi**
Kutunza	50,000 Tsh.
Kuwekeza	125,000 Tsh.
Kutoa	50,000 Tsh.
Matakwa	75,000 Tsh.
Akiba maalumu	125,000 Tsh. + 5000 = 130,000 Tsh.
JUMLA	**430,000 Tsh.**

Mfano Jedwali la 7

Elezea – Ikiwa tumeamua kutunza 50,000 Tsh., kuwekeza 125,000 Tsh., kutoa 50,000 Tsh., kutumia 75,000 Tsh. katika mahitaji na kutunza 125,000 Tsh. kuelekea pikipiki. Tukijumlisha zote hizi tutapata mwishoni 425,000 Tsh. hivyo bado tutakuwa na 5000 Tsh. kwa kuongeza. Tujaribu kuigiza tumeamua kuongeza hiyo katika fungu la pikipiki.

Sasa weka mipango kwa pesa yetu. Angalia baki uliyokuwa nayo katika somo la 3. Iandike hiyo chini. Andika kiasi ambacho ungependa katika maeneo haya. Tena uongeze. Ikiwa jumla imeongezeka sana itakulazimu kutoa baadhi, ikiwa imepungua sana hivyo utaongeza baadhi.

ZOEZI LA BINAFSI

***Maelezo ya Mwezeshaji:** Gawa **Mwongozo wa Wanafunzi**: Hatua za Bajeti 4. Waalike washiriki kukamilisha chati zao na mahesabu.*

Kipindi utakachomaliza bajeti yako ionyeshe kwa wengine na uwaambie watoe ushauri walionao.

REJESHA RIPOTI

***Maelekezo ya Mwezeshaji:** Ukiwa unafanya mapitio ya kukamilisha bajeti hapa chini, ufafanue kwa mfano ulioandika, na uwahamasishe washiriki kupanga kufuata **mwongozo wa mwanafunzi**.*

Naomba tupitie hatua zote:

Hatua 1: Hesabu kipato halisi.(2.1)

Kipato kamili (Jedwali *1)* – Gharama za matumizi *(Jedwali 2)* = Kipato halisi *(Jedwali 3)*

Hatua 2: Hesabu kujua mahitaji yetu. (3)
Gharama za kawaida za kila mwezi (*Jedwali 4)* & Gharama zingine (Jedwali *5)*
(Usisahaku kuweka gharama nyinginezo)

Hatua 3: Hesabu ili kujua tofauti. (3)
Kipato halisi – Gharama za kawaida – Gharama nyinginezo = Jumla kuul *(Jedwali 6)*
Hatua 4: Tumia Salio kwa hekima. (5)
Uamizi uliochukuliwa *(Jedwali 7)*

Kipindi kijacho tutajifunza njia moja ya kutusaidia kukaa katika bajeti yetu.

Somo 6: Utumiaji wa Fedha

Mawazo Makuu

- Tunahitaji utaratibu wa kutunza bajeti yetu.
- Utaratibu wa bahasha ni njia nzuri kwa kutunza pesa yetu.
- Wote pamoja mwanaume na mwanamke uthabiti wa kutunza bajeti.

Vifaa

- Kielelezo: Alama ya Matumizi (1 Seti)
- Kielelezo: Mfano wa bahasha, Weka alama katika utangulizil (1 Seti)
- Bahasha zisizo na alama (10 kwa kila mshiriki)
- Karatasi za kadi ya pesa thamani ya 250.Hakikisha inaweza kupungua kidogo katika matumizi. Unaweza kutumia kadi ya pesa kwenye somo la1, ziada 2500 Tsh. kwa karata zitakazokuwa zimetolewa kama Kielelezo)
- Mwezeshaji-kukamilisha nakala za mfano wa bajeti hatua 1-4 (kutoka somo lililopita)
- Washiriki wawe na nakala zao za bajeti iliyokamilika hatua 1-4 (iliyokamilika somo lililopita)

Utangulizi

Hatua ya kwanza ya kuwa wakili mzuri wa pesa zetu ni kutengeneza bajeti. Ingawa hiyo haitoshi – Tunapaswa kiukweli kufuata bajeti. Mara nyingi ni rahisi kutengeneza bajeti kuliko kuifuata. Ingawaje, kwa kuwa na kiasi na nidhamu inawezekana.

- Kwa sasa unatunzaje pesa yako? Unatumia njia ipi ili kufuatilia vitu tofauti ambavyo unahitaji pesa?

Katika somo hili tutaangalia njia rahisi ya kutunza pesa yetu kupitia utaratibu wa bahasha
Hatua ya kwanza kwa wote wawili mme na mke kuamua uamuzi wa kutunza bajeti. Ikiwa mtu mmoja pekee amejizatiti hivyo utangundua kwa haraka haitawezekana. Pamoja mbele za Mungu, kujitoa na kujaribu kutunza pesa ambazo amewapa kwa hekima na kuzitunza kwa mipango mliyoiweka.

Utaratibu wa Bahasha

KAZI YA KIKUNDI KIKUBWA –Tumia **kielelezo***: Alama na Mfano wa Bahasha ya Matumizi*
Maelekezo ya Mwezeshaji: *Chukua zoezi la mfumo huu wa bahashawakati wote wa mafundisho* ***(****a) – (d) kama ifuatavyo hapa chini.*

Njia bora na rahisi kwa kutunza pesa yako ni utaratibu wa bahasha. Kutumia utaratibu huu, tunagawanya pesa kulingana na bajeti na kuziweka ndani ya bahasha. Hivyo tunatumia pesa ambazo tumeziweka kwa ajili ya matumizi. Kwa kufanya hivyo inatuhakikishia kutozidisha matumizi kwa sababu itatulazimu kutumia tulichokiweka ndani ya bahasha. Ili kuelewa vizuri zaidi, tutaangalia mfano.

Maelekezo ya Mwezeshaji: *Weka kila lebo kutoka* ***kielelezo*** *6: Alama ya Matumizi juu ya sakafu au meza na rejea majadiliano yaliyofanyika chini. Elezea kwamba utajadili alama ya mfuko wa familia. Ambao ni tofauti na sio matumizi, kifupi.*

Mapato Matumizi	Matumizi Kawaida Mwezi	Matumizi Mengine	Mfuko wa Familia

Katika bajeti yetu kumbuka kwamba kuna sehemu tatu tofauti kwa ajili ya matumizi yetu.

1. Mapato matumizi

2. Matumizi kawaida ya mwezi
3. Matumizi mengine ya dharura

Kwa kila aina ya matumizi, tunaweza kuandaa bahasha. Tunahitaji bahasha moja kwa mapato na matumizi, moja kwa matumizi ya mwezi na moja kwa ajili ya kila aina ya matumizi ya dharura (kama vile moja kwa matumizi yote ya shule, moja kwa ajili ya marekebisho, moja kwa ajili ya mavazi na moja kwa ajili ya mengineyo.)

Maelekezo ya Mwezeshaji: *Weka kila bahasha iliyoandaliwa kutoka somo 6* ***Vielelezo****, Mfano A – Mafungu Sita muhimu ya matumizi ya bahasha yaliyochaguliwa, yakiwa mbele ya washiriki.*
Elezea kwamba umeshaandaa bahasha za msingi wa matumizi katika mfano wa bajeti tulioendeleza kabla ya somo.

Sasa, waambie kikundi wachambue bahasha kwenye alama sahihi ambazo umeshaziweka kutoka kwenye alama 6 za matumizi.

- Je, bahasha hizi zaweza kwenda chini ya kila Lebo inayoonesha aina za matumizi?

Mapato Matumizi	Matumizi Kawaida Mwezi	Matumizi Mengine
Mapato matumizi 1,250,000 kwa mwaka	Matumizi Mwezi 285,000 kwa mwezi	Marekebisho 62,500 kwa mwaka
		Mengineyo 25,000 kwa mwaka
		Matumizi Shule 112,500 kwa mwaka
		Mavazi 75,000 kwa mwaka

- Yameonyeshwa wapi kwenye bahasha matumizi mawili ya bajeti ya mengineyo?
    - *Matumizi mengineyo ya mwaka yana bahasha yake inayojitegemea chini ya 'Matumizi Mengine'*
    - *Matumizi ya mwezi yamejumuishwa kwenye jumla ya kiasi cha matumizi ya mwezi.*

Sasa tutaenda kuona namna ya kutumia utaratibu huu.

a) Endeleza Mfuko wa Familia yako

Wakati wowote unapopokea pesa, unapaswa kuiweka katika sehemu maalum (pile). Hii sehemu maalum inaitwa Mfuko wa familia.

Maelekezo ya Mwezeshaji: *weka karatasi ote za pesa ulizoandaa, zenye kiwango cha thamani ya 625,000 Tsh. chini ya Alama ya Mfuko wa Familia.*

Haijalishi uko sehemu gani, unapaswa kutumia bahasha, box lililofungwa, akaunti ya benki au sehemu salama ya kutunza pesa kwa hili.

b) Elekeza matumizi yako ya kawaida ya mwezi

Katika kila mwanzo wa mwezi chukua pesa kwenye mfuko wa Familia na uweke kiasi sahihi ndani ya bahasha ya Matumizi ya Mwezi kila mwezi.

Watu wengine upendelea kuwanya 'kwa mwezi' bahasha, kutofautisha bahasha nyingi kwa kila matumizi ya mwezi, kama vile bahasha binafsi kwa chakula, matumizi ya vifaa vya nyumbani n.k

Maelekezo ya Mwezeshaji: *Ondoa bahasha ya jumla ya matumizi (285,000 Tsh. kwa mwaka) na weka kila bahasha iliyoandaliwa kutoka somo la 6* ***Kielelezo*** *B: Mfano: ongezeko la miezi mitano ya matumizi ya bahasha zilichambuliwa, kama ilivyoonyeshwa chini ya matumizi ya kawaida ya mwezi. Ndipo uwaambie kikundi kujaza kutumia bahasha za kila mwezi kutumia fedha kutoka mfuko wa familia. Je, kutakuwa na ongezeko lolote kwenye ongezeko la gharama za mwezi?*

Mapato Matumizi	Matumizi Mwezi Kawaida	Matumizi Mengine
Mapato Matumizi 1,250,000 kwa mwaka	Miezi Iliyobaki 75,000 kwa mwezi	Marekebisho 62,500 kwa mwaka
Mavazi 75,000 kwa mwaka	Shule 12,500 kwa mwezi	Mengineyo 25,000 kwa mwaka
	Zaka 30,000 kwa mwezi	Matumizi Shule 112,500 kwa mwaka
	Chakula 150,000 kwa mwezi	
	Umeme na Maji 17,500 kwa mwezi	

c) Elekeza matumizi yako mengine ya mwaka

"Bahasha ya mwaka" inatakiwa kujazwa mara moja kwa mwaka. Hii itakuwa baada ya kuwa umepokea kiwango kikubwa cha mapato kwa mwaka, kwa mfano, mara tu baada ya kuvuna mchele. Mapema tu baada ya muda wa mavuno, weka pesa ndani ya bahasha.

Maelekezo ya Mwezeshaji: *Elezea kwamba katika mfano huu ni baada ya kuvuna mchele. Waambie kikundi kujaza kwa mwaka bahasha kwa kwa kutumia pesa kutoka mfuko wa familia.*

d)Kutumia pesa

1. Kutumia pesa kutoka kwenye bahasha pekee

Usiguse mfuko wa familia tena mpaka mwezi ujao. Tumia pesa kutoka kwenye bahasha tu.

Kwa mfano, ikiwa unahitaji pesa kwa ajili ya umeme, fungua bahasha ya utility na kutumia pesa hizo. Kama hakuna pesa zaidi kwenye bahasha, hivyo huwezi kutumia pesa zaidi kwa kitu hicho. Unapaswa kusubiri mpaka mwezi ujao ambapo utakuwa na pesa tena.

Jambo lisiloepukika ni tatizo la dharura, kama vile hitaji la kwenda kwa daktari na kulipia dawa. Hivyo unaweza kuchukua kidogo kutoka bahasha ya mengineyo ili kukidhi matumizi ya dharura. Usitumie bahasha ya mengineyo kulipa kwa ajili ya kitu unachohitaji kwa kujifurahisha mfano kununua nguo mpya. Zitumie kipekee kwa "mahitaji" Tunapaswa kujifunza kuwa na nidhamu na uvumilivu na kusubiri mpaka utakapokuwa na pesa za kununua kitu. Unaweza kuishia na chakula kizuri katika siku ya kwanza ya kila mwezi kukiwa na pesa mpya katika bahasha, lakini wali mkavu katika siku ya mwisho ya mwezi.

Tunapaswa kuwa makini tusichukue pesa zaidi kutoka kwenye mfuko wa familia. Hizi sio pesa za akiba. Kuna mipango kwa ajili ya hizo zote. Ikiwa tutachukua pesa zaidi kutoka mfuko wa familia, hivyo haitakuwepo ya kutosheleza kwa mwaka mzima. Ikiwa tunahitaji pesa kwa kitu cha ziada, hivyo tunahitaji kutafuta njia ya kuingiza pesa ya ziada ili kwamba tuwe nazo. Lakini hatupaswi kuunua mpaka tutakapokusanya pesa ya ziada.

2.Hakikisha unatenga salio lolote kwa hekima
Ikiwa una ziada, unaweza kuandaa bahasha kwa kila hitaji ambalo umepanga katika bajeti yako kwa kutumia pesa iliyobaki, kama vile kutunza, kuwekeza au kutoa.

Maelekezo ya Mwezeshaji : *Weka bahasha ya "ziada" iliyobaki (**Kielelezo**: Mfano wa Bahasha - -Mfano C)tofautisha kwa alama. Karibisha vikundi kujaza kwa kutumia baki ya pesa kutoa Mfuko wa Familia.*

Kutunza 50,000 kwa mwaka	Kuwekeza 125,000 kwa mwaka	Kutoa 50,000 kwa mwaka	Matakwa 75,000 kwa mwaka	Akiba maalumu 130,000 kwa mwaka

Katika mfano huu, kutakuwa hakuna pesa ya kutosha kwa bahasha zote kujazwa kwa usawa. Ingawa, kusudi maalum la kutunza katika mfano huuni kwa pikipiki unayotarajia kutumia kwa biashara, hiyo unashauri kupewa kipaumbele zaidi ya maeneo mengine.

Huu ni mwisho wa mfano wetu wa kutunza matumizi yetu ya nyumbani.

Mkazo

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO
Vipi kuhusu gharama za kipato?

- Kwa nini unafikiri atujaeleza kipengele cha mapato na matumizikwa undani hapa?
    - *Inatakiwa kutunzwa kikamiliffu tofauti kutoka matumizi ya nyumbani.*

Matumizi yako ya kawaida ya mwezi na matumizi mengine ya dharura yalipigiwa hesabu kwa msingi katika mapato matumizi ambayo tayari yalikuwa yamepatikana kwa, kutumia pato "lako halisi".

Yeyote anawajika tena kwa biashara au kuajiliwa, anapaswa kuhakiki kwamba mapato na matumizi yamepatikana kabla pesa haijawekwa kwenye mfuko wa familia.
Unaweza kutumia utaratibu huo wa bahasha kupanga kwa na kusimamia mapato yak o na matumizi vivyo hivyo, lakini zinapaswa kutunzwa tofauti kutoka Kawaida na matumizi mengine ya nyumbani.

JARIBIO LA KIKUNDI KIKUNDI KIDOGO
Maelekezo ya Mwezeshaji: *Karibisha washiriki kuunda vikundi vidogo 3 , kukaa sehemuambayo wataona mfano, Kutakuwa na maswali 7 ya msingi katika mfanohuu.*

Maswali:
1: Ni bahasha ipi ambayo ungetumia kunua chakula?
2: Bahasha ipi ambayo ungetumia kulipia ada ya shule?
3: Katika mfano huu, bahasha ipi ungetumia kwenda nje kwa ajili ya soda mara moja kwa mwezi pamoja rafiki wa karibu?
4: Umemaliza kazi ya ziada ya kibarua kwa siku 2 katikati ya mwezi. Je pesa hiyo utaiweka wapi?
5: Mama yako amepatwa na ugonjwa na anahitaji dawa kwa wiki mbili; Ni bahasha ipi utakayotoa pesa?
6: Utajaza vipi matumizi ya mwaka ikiwa umeingiza kiasi kidogo kwa mwaka mzima?
7: je utafanya nini na na pesa ambayo hujaitumia mwezi huu kwa sababu ulitunza ndani ya bajeti yako mwezi na umebakiwa namengineyo?

Majibu:
1: Matumizi ya kawaida ya mwezi, Bahasha ya chakula
2: Matumizi mengine, Bahasha ya ada ya shule
3: Matumizi ya kawaida ya mwezi, Bahasha ya Mwezi ya Baki
4: Mfuko wa Familia Pile (uchukulie kwamba matumiz na mapato yameshakamilishwa)
5: Inategemeana na kiasi, inaweza ikawa kutoka katika,
a) Matumizi ya Kawaida ya Mwezi, Bahasha ya Mwezi iliyobaki Remaining (kwa sababu bajeti yako inahusisha baadhi ya matumizi mengineyo kwa mwezi)
b) Matumizi mengine, Bahasha ya Mengineyo kwa mwaka.
6: Siku zote kwanza jaza bahasha yako ya matumizi ya mwezi, nandipo ujaze matumizi ya mwaka. Ikifikia hatua ya matumizi ya mwaka kukamilika, ndipo uanze kwanza kuelekeza kwa "kutumia Remainder Wisely" eneo.
7.Utaelekeza kwanza katika 'matumizi mengine' Bahasha ya vitengo ambayo bado haijajazwa, ikiwa zimekamilika kwa mwaka, utaendelea katika "Spending the Remainder Wisely" eneo kulingana na bajeti.

MREJESHO KIKUNDI KIKUBWA CHA TAFAKARI

- Unaweza kuelezea kwa namna gani utaratibu huu ni tofauti na utaratibu unaofanya kwa sasa? Ni kitu gani kinacholeta changamoto kwako?
- Ni kwa jinsi gani utaratibu huu utafanya vitu vyepesi kwako na familia yako?
- Unafikiriaje huu utaratibu utatusaidia sisi kumheshimu Mungu?

Hatua za Utekelezaji

Sasa unaweza kupanga utaratibu wako wa bahasha kwa ajili ya nyumba yako. Anza kwa kuangalia bajeti yako. Andaa bahasha moja kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya mwezi. tena uandae bahasha moja kwa kila matumizi mengine ya mwaka.Ikiwa una ziada, pia unaweza kuandaa bahasha kwa namna ulivyotumia baki yako.
Ikiwa utapenda, unaweza kugawanya tena matumizi yako ya kawaida ya mwezi kama mfano hapa.
Mwishoni, unaweza pia kuandaa bahasha kwa kila mapato na matumizi yako, pale tu unapojua kwa uhakika.

Jaribu kuishi kwa miezi michache katika bajeti kwa kutumia nje ya bahasha. Ikiwa utaendelea na utaratibu bahasha, ndipo utaanza kununua baadhi ya vitu ambavyo umeviweka kwenye orodha ya "matakwa" yako.

Somo la 7: Je tunapata fedha?

****KWA JAMII YA WAKULIMA PEKE YAO**

Mawazo Kuu

- Tunapaswa kujua namna ya kutafuta hesabu ya faida
- Tunaweza kupanga kitu gani chakufanya ikiwa tunapata kidogo au hakuna faida.
- Tunapaswa kutunza kumbukumbu

Vifaa

- Vielelzo: Shamba likiwa na mazao mengi (Picha)
- Mwongozo wa Mwanafunzi: Kuhesabu Faida.
- Ubao na kalamu

Utangulizi

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Tumeshajifunza jinsi ya kubajeti kwa ajili ya familia na kutunza pesa zetu kwa ajili ya matumizi binafsi. Sasa tunakwenda kuangalia matumizi ya biashara. Hii inatakiwa kuzingatiwa kipekee.

Watu wengi wanafanya kazi kwa nguvu, lakini wanapata kidogo au hakuna faida. Tunapaswa kupata muda kufanya hesabu ya faida ili tuwe na uhakika wa kazi yetu ngumu tunayofanya inatulipa vizuri.

Maelekezo ya Mwezeshaji: *Inua juu picha ya* ***Kielelezo*** *7: Shamba lenye mazao mengi. Waulize wanakikundi:*

- Hii ni biashara ya manufaa? Kwa nini au kwanini hapana?
- Inawezekana kusema kutokana na hii picha ikiwa shamba hili linatengeneza faida?
- Unapenda kujua nini ili utuambie iwapo lina faida?

Sio kwamba shamba lina mazao mengi lina maanisha kwamba linatengeneza faida. Kifupi angalia kiasi cha mauzo ulichonacho baada ya kuuza mazo pia hakiwezi kututhibitishia sisi namna kinavyopata faida.

Unapaswa kufanya hesabu rahisi na kuweka kumbukumbu ili kuona kwamba biashara ina mafanikio. Ili kujua ikiwa shamba linatengeneza faida tunapaswa kujua mambo mawili ya msingi.

1. Kiasi gani cha pesa tumepata kutoka kwenye mauzo ya mazao.
2. Kiasi gani cha pesa kilitumika kupanda, kukuza na kuvuna mazao.

Kwa kufanya hesabu ya kutofautisha kati ya hivi viwili, tunaweza kujua iwapo shamba linazalisha faida au hapana.

Maelekezo ya Mwezeshaji: *Gawanya* ***Mwongozo wa Mwanafunzi****: Hesabu ya Faida (4 kurasa). Kwa masomo yaliyobaki, soma na kufanyia kazi maelekezo yalivyoelezwa hapo chini. Andika mfaano wa kwanza juu ya ubao na kufanyia kazi pamoja kwa utaratibi polepole.*

Mfano wa 1: Ana na Biashara yake ya mbogamboga

KIKUNDI KIDOGO CHA MJADALA

Tutamwangalia Ana na biashara yake ya mbogamboga ili tuweze kujifuza zaidi.

Ana anao uzoefu wa miaka tangu aendeshe biashara yake ya kilimo cha mbogamboga katika shamba lake la familia. Ameanzisha shamba lake binafsi la biashara za mbogamboga. Baada ya mavuno yake ya kwanza

Ana akapeleka mboga sokoni na kuuza zote kwa 62,500 Tsh. Alikuwa na furaha sana. Ilionekana kuwa ana pesa nyingi sana.

- Unafikiri kwamba Anna ana biashara ya mafanikio?
    - *Hadi Anna afahamu ikwa amepata faida au hapana, hawezi kujua ikiwa biashara yake ina mafanikio na je aendelee nayo.*

Tutaangalia katika kumbukumbu ya biashara kuona kama amefanikiwa.

Matumizi – Orodhesha vitu vinavyohitajika	**Gharama**
-Mbegu	15,000
-Mbolea	12.500
-Vifaa	10,000
-Sokosehemu ya kuuzia	5000
-Mifuko ya karatasi na kreti	7500
-Tiketi za basi	2500
Jumla	**52,500 Tsh.**
Mapato – Kadilio	**Kiasi**
Jumla	**62,500 Tsh.**

JUMLA MAPATO	**- JUMLA MATUMIZI**	**= FAIDA**
62,500 Tsh.	**- 52,500 Tsh.**	**= 10,000 Tsh.**

Kama tunavyoona, Ana alipata faida - lakini kiasi cha 10,000 Tsh. tu.

MUDA

- Tofauti na kuangalia kiasi gani cha faida amepata, unafikiria kigezo gani kingine anaweza kukiangalia ili aone kwamba anafurahia biashara yake?
    - *Kiwango cha muda alichowekeza kwenye biashara. (Washiriki waandike majibu kwenye karatasi zao)*

Wakati mwingine biashara yenye faida ndogo inaweza kuchukuliwa mafanikio ikiwa kiasi cha muda kinahitajika kutengeneza pesa pia ni kidogo. Ikiwa muda mwingi na nguvu zimewekezwa katika biashara na biashara na biashara inaingiza faida kidogo., hivyo mtu anapaswa kutafakari wazo la biashara.

Msimu wa kwanza kukuwa Ana ulimchukua miezi 4. Ana aliweka kumbukumbu muda aliotumia kufanya kazi kila siku. Wakati Ana ameanza biashara alifikiri kwamba asingetumia muda mwingi kwenye bustani kila siku.Ingawa, mwaka huu, mwezi wa baridi ulikuwa mkavu na Ana alilazimika kufanya zaidi ya kazi ili kumwagia mboga maji. Kupanda na kuvuna pia vilichukua muda mrefu kuliko alivyotegemea na alimwomba binti yake amsaidie.

Ana alikadilia kwamba muda wote alioweka wa biashara kuanzia kupanda hadi kuuza, pamoja na muda kwenda sokoni ulikuwa ni masaa 12.5 kwa mwezi. Na hii ikafanya jumla ya masaa 50 kwa

Msimu kuongezeka (Idadi ya miezi):	4
Masaa / Mwezi:	12.5
Jumla (Masaa/Miezi x idadi ya miezi)	50
Faida / Idadi ya miezi, Masaa	200 Tsh.

msimu mmoja wa kupanda. 10,000 Tsh. ukigawa kwa masaa 50 unapata dola 200 Tsh. kwa saa. Sasa ni bayana kwamba 10,000 Tsh. ni kidogo sana kwa kazi atakayoifanya.

Ana anahitaji kupanga namna atakavyopata faida nzuri msimu ujao. Anatakiwa kujaribu kupunguza garama. Ingawa anaweza kutumia mbolea itakayomsaidia kukuza zaidi au kutafuta njia kuvuna mbegu zake mwenyewe.Ikiwa Ana hawezi kupunguza garama katika biashara yake ya mbonga, itakuwa na faida zaidi kwake akijaribu kufanya biashara nyingine tofauti kwa pamoja.

Kwa bahati mbaya, biashara nyingi ni kama mboga za Ana. Tunafanya kazi kwa bidii na tunashindwa kutambua kwamba tunapata pesa kidogo sana.

Mfano wa 2: Nguruwe za Paulo

ZOEZI LA KIKUNDI KIKUBWA

Tunaweza kutumia chati kama ya Ana kufanya hesabu ikiwa tunatengeneza faida. Kabla hatujazingatia biashara yetu tuangalie tena biashara mbili zaidi.

Maelekezo ya Mwezeshaji : *Tazama kwenye chati isiyojazwa kwenye kablasha la Nguruwe za Paulo. Zungumzia hatua zote. Hakikisha wanaelewa kwamba jumla ndogo ilitumika kwa matumizi na mapato.*

Paulo alikuza nguruwe. Amekuwa akikuza nguruwe kwa miaka mingi lakini anataka kuwa na uhakika kwamba anapata pesa.Kwa kipindi cha miezi sita iliyopita amekuwa makini kuweka kumbukumbu zote za matumizi ya nguruwe wake. Leo ameuza nguruwe na sasa anataka kufanya hesabu aone ikiwa amepata faida kwa biashara yake ya nguruwe.

Tafazali kamilisha chati ya Paulo katika kablasha (Vitini)

- Paulo alipata faida?

Hatua 1. Jina la Mradi	Nguruwe za Paulo
Hatua 2. Ukubwa wa Mradi	Siku 100
Hatua 3. Matumizi – Orodha ya vitu vinavyohitajika	**Gharama**
Nguruwe 2	100,000
Chakula cha nguruwe 2	125,000
Chanjo	2
Jumla ya Matumizi	**230,000 Tsh.**
Hatua 4. Mapato - Makadilio	**Kiasi**
Jumla Mapato	**700,000 Tsh.**

Kumbuka: Hesabu ya mapato: [kiasi / kg] x [uzito wa nguruwe] x 2 [nguruwe] (4,375 x 80 x 2 = 700,000)

Mapato	**- Matumizi**	**= Faida**
700,000 Tsh.	- 230,000 Tsh.	470,000 Tsh.

Muda	
Msimu wa Kukuzia (idadi ya siku)	100
Faida / na. siku	4,700 Tsh.

Example 3: Kibanda cha nguo cha Yohana

PAMOJA NA MWENZAKO

Kama Paulo, Yohana alitaka kuwa na uhakika kwamba duka la ushonaji linafanya vizuri. Pia aliweka kumbukumbu ya miezi 6 iliyopita lakini alipata kuchangayikiwa. Hakuwa na uhakika kitu gani aandike na kitu gani asiandike.

Maelekezo ya Mwezeshaji: *Wagawe washiriki kiwango cha wawili. Wanaweza kufanya kazi pamoja kutumia karatasi.*

Fuata hatua hizi kumsaidia Yohana kufanya hesabu ya faida:
Hatua ya 1: Kata chochote ambacho hakihusiani na biashara ya ushonaji wa nguo.
Hatua 2: Pitia orodha na kubainisha kipato chochote ambacho umepata kutokana na duka la nguo – weka katika sehemu ya mapato kwenye karatasi.
Hatua 3: Pitia na ubaini matumizi yote. Weka matumizi kwenye upande wa matumizi katika karatasi.
Hatua 4: Kama ulivyofanya kwa Paulo, tumia matumizi na faida kuona ikiwa Yohana alipata faida.

Kitabu cha kumbukumbu cha Yohana

Kununua nguo za kuuza	1,250,000	Kuuza Nguo	1,250,000
~~Ada ya Shule~~	~~750,000~~	~~Chakula kwaajili ya familia~~	~~125,000~~
~~Begi la Shule~~	~~100,000~~	Kuuza nguo	1,000,000
Kodi ya Paango la duka	250,000	~~Kuninua zawadi kwaajili ya Siku kuu~~	~~750,000~~
Kuuza Nguo	1,250,000		

Hatua ya 1. Jina la Mradi	Mavazi ya Yohana
Hatua ya 2. Ukubwa wa Mradi	6 Miezi
Hatua ya 3. Gharama- Orodha ya vitu vinavyohitajika	**Gharama**
Kununua mavazi kwaajili ya kuuza	1,250,000
Gharama za Pango la Duka	250,000
Jumala ya Gharama	**1,500,000**
Hatua ya 4. Kipato - Makadirio	**Kiasi**
Uuzaji wa nguo	1,250,000
Uuzaji wa nguo	500,000
Uuzaji wa nguo	1,000,000
Jumala ya Kipato	**10,800,000 Tsh.**

Kipato	**- Gharama**	**= Faida**
10,800,000 Tsh.	-1,500,000 Tsh.	9,300,000 Tsh.

Muda

Uwezo wa Mradi (Miezi)	6
Faida / idadi ya Miezi (9,300,000 / 6 = 1,550,000)	1,550,000 Tsh.
Faida / idadi ya miezi / 30 Siku (1,550,000 / 6 = 51,667)	51,667 Tsh.

Kufanya kazi nje ya Gharama

ZOEZI BINAFSI

Tunapaswa kuhakikisha kuwa mradi wetu hautafanana na ule wa Ana, badala yake uwe kama wa Paulo.Angalia jedwali la mwishao katika Nakala yako.

Hatua ya Kwanza: Chagua ni mradi upi ututumia kuhesabu faida. Usihusishe njia zingine zinazotupatia kipato (kv. Kuuza Mchele, Kuuza Mbogamboga, Kuku, na nguruwe). Katika jedwali hilo, chagu chanzo kimoja tu cha uchumi.

Maelekezo kwa Mwezeshaji: *Hakikisha kila mwanakikundi amechagua mradi wake wa kufanya.*

Hatua ya Pili: Eleza muda utkaotumia katika Mrdi huo. Kwa mfano, Ana alitumia muda wa miezi 4 kwa Sababu ndio muda aliotumia tangu kupanda mbogamboga hadi hatu aya kuvuna na kuuza. Paulo alitumia muda wa miezi 6 kwasababu huo ndio muda aliotumia kutunza nguruwe wake tangu wakiwa wadogo hadi walipokuwa wakubwa. Kama unalima mpunga, ni vyema uhesabu muda tangu unapoandaa shamba lako hadi utakapovuna na kuuza mpunga wako. Kama wewe kufanya kitu kama kushona nguo au kuuza supu, basi unaweza kutumia wiki moja au mwezi mmoja.

Maelekezo ya mwezeshaji: *Uwaruhusu washiriki kufanya hatua ya 1 na 2 kabla ya kufanya hatua ya 3 na 4.*

KIKUBDI KIKUBWA CHA KUBADILISHANA MAWAZO

Hatua ya 3: Usitumie gharama za Mradi. Kabla ya kushughulika na jambo hili, ni vizuri kwanza kufikiri ni kipi kinahitajika ili kuanza mradi huo. Kujaribu kufikiria kila kitu ni jambo gumu tena tunaweza kusahau upesi. Ili kurahisisha kazi hii, hebu sasa tuangalie mfano ufuato:

> Lili anashughulika na ufugaji wa kuku. Katika kuandaa mradi wake, aliorodhesha mahitaji yote ya mradi wake kwa siku nzima. Alijiuliza maswali binafsi juu kutunza mradi wake kwa siku nzima. Kwa mfano, kama asubuhi Lili anatembelea banda lake la kulishia kuku. Je, liko wapi?Liko karibu na nyumba yake?Ikiwa liko mbali atafikaje huko?Je, atalipia kodi ya kupanga?Baadaye alijiuliza tena bandani.Atafanya nini kwanza?Analisha kuku. Atatumia nini? Atapata wapi chombo cha kulishia? Kinagharimu kiasi gani cha fedha?Kuku wanahitaji kupata nini ili wawe na afya?Je anatakiwa kumwajiri mtu mwingine kumsaidia katika mradi wake?Baada ya kufanya haya yote, Lili alikuja na orodha ya mahitaji yote ya mradi wake.

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Kama kikundi, hebu orodheshaubaoni mahitaji ambayo ni muhimu kwa kuanza bishara.*

Biashara hutoafutiana, hivyo unapaswa kufikiri kwa uangalifu ni kitu kipi unahitaji kwa ajili ya mradi wako.

ZOEZI LA MTU BINAFSI

Orodhesha mahitaji unayodhani ni muhimu kwa mradi wako. Ongea na watu wengine walio na mradi unaofanana na mradi wako ili kuangalia gharama zote.

Wakati huu tunapaswa kuangalia makadirio ya gharama za vitu vinavyohitajika kwa ajili ya Mradi. Pitia orodha ya vitu vilivyo ordheshwa na kuona kila kitu kinagharimu kiasi gani. Ikiwa hujui bei halisi ya kitu hicho, basi jaribu kukadiria tu.

Utagundua kuwa baadhi ya vitu katika orodha vinahitajika kila wakati unapozalisha kitu flani wakati vitu vingine vinahitaji kununuliwa mwanzoni mwa mradi. Ikiwa umeshalipia gharama za vitendea kazi na ardhi inayohitajika kwaajili ya biashara yako iko tayari kwaajili ya biashara yako, hutahitaji kuuganisha gharama za vitu hivyo kwenye orodha ya manunuzi yako.

Htaua inayofuata ni kuongeza gharama hizo ili kupata jumla yote. Andaika gharama zote hizo kwenye karatasi unayofanyia kazi.

Kuhesabu Faida

Hatua ya 4: Hesabu ili ujue ni faida kiasi ulichoingiza kutokana na mradi. Kwa Bashara nyingi jambo hili siyo gumu maana unaweza kuuza bidha zako kwa awamu moja kama vile baada ya mavuno ya mpunga kile kiasi ulichoingiza baada ya mavuno. Jaribu kuhesabu wastani ulioupata kutokana na mauzo. Andika jumla ya mapato kwenye karatazi unayofanyia kazi. Kumbuka kinachotafutwa hapa ni mauzo kwa kipindi ulichokuwa umeorodhesha kwaajili ya biashara yako.

Ikiwa hutaki kuuza mazao yako kama vile Mpunga, basi tunza kwaajili ya chakula lakini Fanya makadirio ikiwa ungenunua mpunga huo, ungetumia kiasi cha fedha. Kwa mfano, kama ulivuna Kg 500 na hukuzitumia kama chakula ungenunua kila 1kg kwa dola 50, na uhesabu hivyo kwa 500kg ili kujua kipato chote. Ni muhimu sana kuhesabu kipato chetu ili kujua gharama zote na kuona kama mpunga tuliopata ni hasara ili kuona kama ni bora kununua badala ya kulima.

Hatua ya 5: Kwa sasa tunaweza kujua kama biashara yako imeleta faida au la. Fanya mahesabu kwa kutumia zile jumla ili kujua mapato.

- Je, biashara yako imekuletea faid?

UMUHIMU WA KUTUNZA KUTUNZA KUMBUKUMBU

Wakati mwingine unapopanda mazao yako au kununua wanyama wapya baadae tunza kumbukumbu za ghaama za manunuzi ili ujue kama mradi wako umekuletea faida au hasara. Muda mwingine makadirio yetu yanakuwa na makosa, hivyo ni vizuri kutunza kumbukumbu zote kadri iwezekanavyo. Ikiwa umechanganywa katika kuordhesha kumbukumbu hizo, basi andika kila kitu unachofikiri kinaweza kuwa na uhusiano kisha uliza mtu mwingine akusaidie kufanya mahesabu baadaye.

HATUA ZA KIVITENDO

Ikiwa una biashara nyingi, itakuwa ni vizuri kurudia zoezi hili kwa kila biasha ra uunayoifnya.

Mwombe mwanafamilia au rafiki yako kukusaidia kuangalia makadirio ya na kukusaidia kubuni njia zitakazosaidia kuinua kipato chako.

Somo la 8: Gharama na matokeo ya madeni

Mawazo Makuu

- Kuna hasara nyingi zinazotokana kuwa na madeni siyo tu kifedha.
- Nahitaji kuhesabu riba kwa deni
- Nahitaji kuelewa aina ya mkopo
- Madeni yanaweza kuwa ya manufaa; hivyo ninapaswa kuweka mkakati wa ulipaji kutoka kwenye biashara yangu au mapato.

Vifaa

- Mwongozo wa Mwanafunzi Sehemu A au B *(Chapa sehemu muhimu inayohusu mada yako na kisha ugawanye kwa kila kikundi kidogo)*
    - Sehemu **'A'** inahusu jamii ya wakulima: inahusu uuzaji wa mazao mapema; haijumuishi malipo ya kiwanja.
    - Sehemu **'B'** inahusu jamii iishiyo mjini: inajumuisha malipo ya majendo; haijumuishi uuzaji wa mazao mapema.
- Washiriki wote wanahitaji karamu na karatasi
- Vikokotoo (Calculator) au simu za mkononi kwajili ya kufanya mahesabu.
- Ubao au karatasi kubwa na kalamu za kuandikia ili kuonesha mfano.

KUMBUKA: SEHEMU ZA WATU WA VIJIJINI NA MIJINI ZILIZOONYESHWA

Utangulizi

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

- Kwa nini watu wanadaiwa madeni?
- Je, watu hununua kitu gani hasa kupitia madeni?
- Je, kuna faida gani katika madeni?
- Je, kuna hasara zipi katika madeni?
    - *Tunaweza kujikuta tukiishia katika kukopa fedha nyingi kwa mfu flani.*
    - *Deni linaweza kuwa mzigo unaosababisha sisi kutokuwa na vitu vya kutosha katika siku zijazo.*
    - *Deni linaweza kutuletea hali ya kutumia kuliko vile tulivyo navyo.*
    - *Deni linaweza kusababisha sisi kutokufikiria matokeo ya maslahi yetu.*
- *Unaweza kufikiria mtu yeyote ambaye ameweza kutumia madeni vizuri?*
- *Unaweza kufikiria mtu yeyote ambaye aliteseka kwa sababu ya deni?*

Mara nyingi madeni yanagharimu- msongo wa mawazo, hofu, mifarakano katika ndoa, kutokupata usungizi usiku, nk. Katika somo hili, tutajikita zaidi upande wa matokeo ya madeni kifedha. Walakini, hatupaswi Kamwe kufikiri kuwa haya tu ndiyo matokeo pekee ya madeni.

Kuhesabu Riba

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Maealekezo kwa mwezeshaji: *Andika ubaoni mifano majedwali yafuatayo ili wa wanadarasa waweze kuona.*

Kwanza, ni lazima tujue jinsi ya kuhesabu riba ambayo ndioyo ziada itakayotumika kama malipo ya fedha inayodaiwa.

Kama tunatumia kalamu na karatasi:

Chukua kiwango cha mkopo, mfano, 250,000. Kata sifuri mbili, mfano, 250,0~~00.~~ = 1 uzidishe kwa kiwango cha ribamfano, asilimia 6%. 2500*6 = 15,000 Tsh. ambazo ndio riba.

250,0~~00.~~ = 2500 2500 x 6 = 15,000 Riba.

Kama tunatumia Kikokotoo au Simu:
Chukua Kiwango cha mkopo. Gawanya mara 100. Kisha zidisha kwa kiasi cha riba.
Mfano, 25,000 / 100 = 2500*6 = 15,000

25,000 / 100 = 2500 2500 x 6 = 15,000 Tsh. Ndiyo

Katika mfano huu, kiasi cha 15,000 Tsh. ndizo fedha ambazoi ni malipo ya ziada kwa mkopo kama gharama ya fedha tulizokopa.

MMOJA MMOJA AU KIKUNDI
Fanya zoezi hili kwnye karatasi nyingine sasa:

Maelekezo ya mwezeshaji: *Andika kiwango cha riba. Wakati washiriki watakapokuwa wamemaliza kufanya mahesabu, ongeza kwenye majibu.*

8% ya riba ya 1,250,000 Tsh. = 100,000 Tsh. 4% ya riba ya 175,000 = 7,000 Tsh. 12% ya riba ya 2,500,000 = 300,000 Tsh. 10% ya riba ya 500,000 = 50,000 Tsh. 6% ya riba ya 1,000,000 = 60,000 Tsh.

Mkopo wowote umepangiliwa kulingana muda wake. Hivyo, ili kuhesabu ongezeko la riba halisi katika mkopo, unapaswa kutambua aina ya mkopo uliotolewa na ni kwa muda upi.

Aina mbili za Mikopo

KIKUNDI KIKUBWA CHA MFANO
Mara nyingi kuna aina mbili tu za mkopo.
Aina ya Kwanza: Unalipa riba kila mwezi kulingana na kiasi ulichokopa. Hii inaitwa Riba Rahisi ambayo tayari umekwisha kufanya hesabu zake hapo juu. Aina ya pili: Unalipa riba kila mwezi kwenye kiwango kilichokopwa. Hii inaitwa riba ngumu.

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Onesha mfano uliopo hapo chini kwa wanadarasa ili kulinganisha utofauti uliopo kati ya aina mbili za mikopo.*

Mfano: 10% riba ya 750,000 Tsh. ya mwezi kwa miezi 4:

<u>Aina ya Kwanza: Riba kwenye kiwango kilichokopwa kwa kila mwezi (Riba rahisi)</u>

Ikiwa riba hii ni kiasi cha kile kilichokopwa basi jumla yake ni

- 10% riba ya 750,000 = 75,000 Tsh.
- 75,000 x 4 miezi = 300,000 jumla ya riba
- **Kiasi kamili kinachopaswa kulipwa ni 300,000 + 750,000 (Mkopo halizi) = 1,050,000 Tsh.**

Riba rahisi (10%) 10% riba ya 750,000 = 75,000 Tsh. 75,000 x 4 = 300,000 jumla ya riba 750,000 + 300,000 = 1,050,000 jumla itakayolipwa

Aina ya Pili: Riba kwenye kiasi kamili kwa mwezi (riba ngumu)

- 10% riba ya 750,000
- Mwezi 1 riba = 75,000
- Jumla ya mwisho wa mwezi 1 = 825,000
  (75,000 riba +750,000 mkopo)
- Mwezi 2 Riba = 82,500
- Jumla ya mwisho wa miezi 2 = 907,500
  (82,500 riba +825,000 Jumla ya mwezi 1)
- Mwezi wa3 Riba = 90,750
- Jumla ya mwisho wa miezi 3 = 998,250
  (90,750 Riba +907,500 Jumla kwa miezi 2)
- Mwezi wa 4 riba = 99,825
- **Jumla ya mwisho wa mwezi wa 4 = 1,098,075**
  (99,825 Riba + 998,250 Jumla ya mwezi 3)

Riba ngumu (10%)	
Mwanza	750,000
Riba	75,000
Mwisho wa mwezi mmoja	825,000
Riba	82,500
Mwisho wa mwezi wa miezi 2	907,500
Riba	90,750
Mwiaho wa miezi 3	998,250
Riba	99,825
Mwisho wa miezi 4	1,098,075

Sasa linganisha jumla kuu ya mwishio kwenye aina ya kwanza (Riba rahisi na ile aina ya pili (riba ngumu). Katika mfano wa kwanza, utaona jumla kuu ya kiwango kinacholipwa ni 1,050,000 Tsh. Katika mfano wa pili utaona jumla ya kiwango kitakacholipwa ni 1,097,500 Tsh.

Kama unavyoweza kuona aina ya pili yaani riba ngumu, utapaswa kulipa riba nyingi. Hebu fikiriu ikiwa mkopo huu ni wa mwaka mmoja badala ya miezi 4.

- Jumla ya Riba Rahisi baada ya mwaka 1 = 1,650,000 Tsh.
- Riba ngumu baada ya mwaka 1 = 2,355,000 Tsh!

Kwa vyovyote, hupaswi kuchukua mkopo wenye riba ngumu, lakini kama utapenda kufanya hivyo, ni vizuri kumwomba mtu mwingine akusaidie kuhesabu gharama zake kwanza.

Riba Rahisi

MMOJA MMOJA AU WAWILI WAWILI

Kwa muda huu hebu fanya mazoezi ya hii mifano ya riba:

Maelekekezo kwa mwezeshaji: Andika mifano hiyo ubaoni. Wakati washiriki watakapomaliza kufanya zoezi lao basi ongeza kwenye hesabu na majibu.

- Je, jumla kuu ya Riba ni ipi katika mifano hiyo?

7% riba ya 7,500,000 kwa miezi 3	= 525,000 x3	=1,575,000 Tsh.
6% riba ya 5,000,000 kwa miezi 10	= 300,000x10	=3,000,000 Tsh.
12% riba ya 12,500,000 kwa miezi 2	= 1,500,000x2	=3,000,000 Tsh.
10% riba ya 6,250,000 kwa miezi 8	= 625,000x8	=5,000,000 Tsh.
8%riba ya 10,000,000 kwa miezi 6	= 800,000x6	=4,800,000 Tsh.

Riba Ngumu – JAMII YA WATU WA MJINI TU

KIKUNDI KIKUBWA CHA ZOEZI

Riba ngumu, ni yale malipo ya riba kwenye kiwango kilichokopwa pakoja na nyongeza ya riba ya kila mwezi.

Hapo tunahesabu moja kwa moja asilimia ya riba, kuiongeza kwenye mkopokupata jumla kuu mpya na kuendelea kufanya hivyo kiuila mwezi.
Heabu tupitie tena mfano.

Ni vizuri kutumia Kikokotoo (calculator) kuhesabu riba ngumu

Lakini pia unaweza kufanya hesabu za riuba ngumu kwa kutumia namba zifuatazo.

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Andika namba kwenye jedwali ubaoni ili kila mmoja aweze kuona. Uwaulize 13% na 4% itakuwa ngapi.*

Iki kufanya mahesbu, unachukua jumla kuu ya mkopo na kuizidisha na namba inayoonyeshs riba. Baadaye unazidisha na namba hiyo kwa kila mwezi kwa kipindi cha mkopo. Hii itakupatia jumla kuu ya kiwango kitakacholipwa.
Baada ya hatua hiyo, gawanya jumla kuu ya mkopo ili kupata kiwango cha riba itkayolipwa.

Maelekezo ya mwezeshaji: *Chora mfano ufuatao ubaoni*

4% =??
5% = 1.05
6% = 1.06
7% = 1.07
8% = 1.08
9% = 1.09
10% = 1.10
11% = 1.11
12% =1.12
13% = ??

Kwa mfano, kama unataka kuhesabu riba kwenye mkopo wa 200,000 kwa asilimia 8% kwa miezi 3:

- 2,000,000 * 1.08 *1.08 *1.08 = 2,519,424 (Jumla ya gharama za marejesho)
- 2,519,424 – 2,000,000 = 519,424 (Riba)

ZOEZI KWA KIKUNDI KIDOGO

Hebu sasa hesabu kiwango hicho hicho cha mkopo kutoka kwenye Riba Rahisi kama ulivyofnya hapo mwanzo.

- Je, jumla kuu ya riba rahisi kwa kila mfano kati yah ii iliyopo?

Majibu ya Riba Ngumu

7% riba ya 7,500,000 kwa miezi 3 = [Jumla kuu itakayolipwa] 9,187,823– [Jumla kuu ya kiwango cha mkopo] 7,500,000 =1687,823

6% riba ya 5,000,000 kwa miezi 10=	8,955,000 – 5,000,000 =	3,955,000 Tsh.
12% riba ya 1,250,000 kwa miezi 2 =	1,568,000 – 1,250,000 =	318,000 Tsh.
10% riba ya 6,250,000 kwa miezi 8 =	12,180,000 – 6,250,000 =	5,930,000 Tsh.
8% riba ya 10,000,000 kwa miezi 6 =	15,867,500 – 10,000,000 =	5,867,500 Tsh.

Maelekezo ya mwezeshaji: *Siyo lazima wafaulu kujibu kwa usahihi maswali yote. Jambo la msingi kwamba wamejifunza kuwa riba ngumu maana yake ni kukutana na hali ngumu katika kila mwezi.*

- Je, kunautafauti upi wa majibu ya riba rahisi? Je, ni yapi yametofautiana?
    - Yako juu sana
    - Je, Mkopo wenye kipindi kirefu uko tofaiti zaidi?

Ikiwa unahitaji kuchukua mkopo wenye riba ngumu, hebu jaribu kuufanya uwe mfupi na ulipe kwa haraka iwezekanavyo.

Mikopo itokanayo na mauzo ya mapema – JAMII YA WAKULIMA PEKEE

ZOEZI LA KIKUNDI KIKUBWA

Madeni mengi hayatokani na fedha tasilimu, bali ni wakati tunapouza mazao yetu. Ili kujua deni, ni lazima tutoe gharama za mauzo halisi. Hapo unaweza kugundua kwamba, mtu anayenunua anajipatia faida kubwa mno kuliko anyeuza.

Kwa kiasi kikubwa, bei wanayokupatia ni chini ya bei ambayo wangetarajia kukupatia sokoni.
Kwa mfano: Unauza kilo 1,000za Kahawa mapema kwa bei ya 3750 badala yake baada ya mavuno ungeuza dola 5000 Tsh.

Gharama za deni

- Fedha iliyopokelewa mapema = 3750 *1,000za = 3,750,000 Tsh.
- Fedha ambayo ungeipokea baada ya mavuno = 5000 * 1,000kg = 5,000,000
- Gharama za deni = 1,250,000 Tsh.

Hebu tufanye mfano mwingine kama kikundi: Unauza kilo 2,000 za Kahawa mapema kwa dola 1.4 badala yake wakati wa mavuno ungeuza dola 2.

Gharama za deni

- Fedha iliyopokelewa mapema = 3500* 2,000za = 7,000,000 Tsh.
- Fedha ambayo ungepokea baada ya mavuno= 5000 * 2,000za= 10,000,000 Tsh.
- Gharama za deni= 3,000,000 Tsh.

Ikiwa unaamua kuuza mazao yako mapema, hakikisha unapata bei ya juu, lakini usirudie kufanya hivyo tena.

Kulinganisha aina ya gharama z madeni

Kuna aina mbalimbali za madeni unayoweza kuingia. Kupitia hatua hii, unaweza kuangalia baadhi ya aina hizi.

ZOEZI KATIKA KIKUNDI KIDOGO

Maelekezo kwa Mwezeshaji: *Tengeneza makundi madogo madogo ya washiriki kati ya watu 3-4; hakikisha kila kikundi kina mtu mwenye utaalamu wa mahesabu. Wagawie nakala za* ***Mwongozo wa Mwanafunzi*** *Somo la 8: Uchaguzi A au Uchaguzi B.*

Kama unahitaji kukopa fedha. Jiulize katika kikundi ni uchaguzi upi utautumia.

Unatakiwa kuwa na 1,250,000 ili kununua mbolea na mchele wa ziada. Hivyo unaweza kuchagua:

1. Kuuza mazao yako mapema. Uza mavuno yako (1200za) kwa 3750 kwa kilogramu badala ya 5000 kwa kilogram.
   Faida iliyopo = 1200kg*5000 = 6,000,000 Tsh.
   Kiwango kilichopatikana = 1200za*3750 = 4,500,000 Tsh.
   Gharama za deni= 6,000,000 – 4,500,000 **= 1,500,000 Tsh.**
2. Unakopa 1,250,000 kwa miezi mitano na kulipia riba ya asilimia 10% riba ya kiwanja
   Jumala kuu ya mapili 1,250,000 * 1.1 * 1.1 * 1.1 * 1.1 *1.1 = 2,013,137.50 Tsh.
   Gharama za deni = Jumla ya marejesho – kiasi cha mkopo = 2,013,137.50 – 1,250,000 **= 763,137.50**
3. Unakopa 1,250,000 kwa miezi mitano kisha unalipa riba asilimia 12% riba rahisi.
   Gharama za deni = 1,250,000 * 12% * 5 **= 750,000 Tsh.**
4. Unakopa 1,250,000 na kukubali kurudisha 2,000,000 ndani ya miezi 5.
   Gharama za deni = 2,000,000 – 1,250,000 **= 750,000 Tsh.**

TAFAKARI JUU YA KILICHOPITA

- Ni uchaguzi upi ambao kundi lako limeuchagua? Jadili
- Unawezaje kuutumia katika familia yako au familia nyingine katika jamii yako?
- Je, kuna aina yoyote ya mikopo inayojulikana katika eneo hili?

Maelekezo ya Mwezeshaji: *Waulize wanakikundi wataje baadhi ya mifano inayoonyesha mikopo ya kawaida pamoja na riba zake. Kwa pamoja wanaweza kuhesabu gharama za deni kutokana na mifano waliyoitaja.*

Je, ni lini tunapaswa kutumia deni?

KIKUDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Biblia haijaeleza wazi ni lini tunapaswa na hatupaswi kutumia deni. Lakini imeweka maelekezo mengi yanayoweza kutusaidia sisi tuweze kufikiri kwa hekima kamani vizuri au vibaya kutumia deni.

Soma mistariifuatayo. Kulingana na mistari hiyo, unageto a ushauri gani kwa mtu juu a matumizi ya fedha?

- Luka 12:15
- Mhubiri 4:7-8
- Mithali 21:17
- Yakobo 4:3
- Warumi 13:8
- Mitahali 22:7

Biblia hutuonya wazi kuwa hatupaswi kutafuta mali. Tunakumbushwa kuwa maisha siyo tu kuwa na mali.Ni bora kuishi maisha ya kawaida kuliko kuwa na mali nyingi na kusongwa na mikopo. Tunatakiwa kuilinda mioyo yetu dhidi ya ulafi na tamaa.

- Je, niwakati upi deni halipaswi kutumiwa? Ni wakati upi deni halipaswi kutumiwa?
    - *deni haipaswi kutumika kununua vitu ambavyo ni kwa ajili ya furaha au maisha ya starehe zaidi, kama vile pikipiki, T.V., au simu ya mkononi. Wakati tunapoingia katika madeni kwa kununua mambo ndipo tunapofanya mambo katika utaratibu mbaya. Tunatamani kuwa na kitu kizuri sana, lakini hatuko tayari kufanya kazi kwanza. Huu unaitwa Uchoyo. Pikipiki mpya au nyumba mpya siyo vitu vibaya, bali tunapaswa kuwa wavumilivu kutafuta fedha za mahitaji haya badala ya kuingia madeni kwa kukopa. Tunapokopa fedha kwaajili ya kulipia kitu flani, tunapaswa kulipia riba na wakati huohuo tutakuwa tumejiweka chini ya utumwa wa mfu flani. Biblia hutuonya kwamba hatupaswi kudaiwa kitu chochote (Warumi 13:8, Mithali 22:7).*

Tunapaswa kuweka mpango mzuri wakati wa kuandaa miradi yetu, mpango utakaoonyesha ni jinsi gani tutalipa deni hata kabla ya kwenda kukopa na kuwekeza. Unapaswa kugundua ni kiasi gani cha faida utapata kutoka katika mradi wako ili utoe kiasi cha mkopo na riba. Kwa maneno Mengine, moja ya gharama katika mpango wa biashara yako ni ile gharama ya deni.

Je, bado unajitahidi kutafuta fedha za kutosha na kuziona kama kitu cha thamani sana?

HATUA YA KIVITEDO

PAMOJA NA MWENZA

Mwombe Mungu na kumwambia akusaidie usiwe na tamaa ya mali usiyokuwa nayo na usiyoihitaji. Umshukuru Mungu kwa mali alizokupatia.

Somo la 9: Kujiondoa katika Deni

Mawazo Makuu

Tunawezea kujiondoa katika deni ikiwa:

- Tutachukua hatua ya kutubu na kuonyesha mabadiliko
- Tutajitoa nia zetu sasa, ili kuwa uhuru
- Tutauza vitu visivyo na umuhimu
- Tutakuwa wabunifu na kuweka mpango wa mabadiliko madogo ya kulipa madeni yaliyopo
- Tutaomba na kutumaini msaada wa Mungu

Vifaa

- Mwongozo wa mwanafunzi: Jinsi ya kuondokana na Deni
- Karatasi kubwa au ubao kalamu za kufanyia mifano
- Mbegu 10, maharage au mawe

Utangulizi

KIKUNDI KIKUBWA CH MAJADILIANO

- Je, hadi muda huu unadhani ni asilimia ipi ya watu katika jamii hii wako chini ya utumwa huu wa deni?
- Je, hadi muda huu, unadhani ni asilimia ipi ya watu katika kanisa lako wanaishi chini ya mzigo mzito wa deni?
- Je, unadhani inawezekana wa kumaliza madeni yote? Kwa nini?
- Je, unatoa msaada gani kwa mtu yeyote kuhusu kuondokana na madeni?

Kumbuka watu wengi, wanakabiliwa na madeni, na wanahitaji kujiondoa katika madeni hayo.

Jinsi ya kuondokana na deni

KIKUNDI KIKUBWA CH MAJADILIANO

1. Tutaungama dhambi zetu na kuamua kubadilika

Tambua kuwa hujamatii Mungu ikiwa matumizi yako hayajawa mazuri. Mungu ni mwenye rehema kwao wanaotubu dhambi zao na kubadili njia zao. Biblia inase, “Afichaye dhambi hatafanikiwa; bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema” Mithali 28:13.

Wakati tunapotubu, pia tunapaswa kufanya maamuzi ya kutokuendelea kuwa katika madeni.

VIKUNDI VYA WATU WAWILI WAWILI

- Kwa wakati mmoja kila mtu amshirikishe mwenzake jinsi alivyopokea rehema za Mungu au wakati ule alipotubu juu ya jambo flani ukapokea Amani ya Mungu ikiwa ni ya hatua ya mabadiliko.
- Fikiria juu ya mfano wowote maishani mwako pale ulipoamua kujitoa kwa jambo au kazi flani. Je, unaweza kueleza ugumu au urahisi uliokutana nao? Je, ni kitu gani kilitokea katika hatua hiyo?
- Je, unawezakutumia maauzi hayo kujitoa katika kuondokana na madeni?

2. **Tutajitoa nia zetu, ili tuweze kuwa na uhuru**

Unaweza kuwa unaishi kwa furaha zaidi kwa muda. Tafakari kwa uangalifu mkubwa juu ya manunuzi yako makubwa. Usinunue vitu usivyovihitaji kwa wakati huo. Usijaribiwe kuuza mavuno yako mapema, au yaliyomo gharani mwako kwa gharama ya chini kwa kigezo cha kupata fedha. Ishi kwa uangalifu kulingana na bajeti yako na uwe mvumilivu ili uuze mavuno yako wakati utakapowadia au kama ghala lako la kutunzia kuwa zaidi ya kiwango ulichokusudia. Kwa njia hiyo, kipato chako kwa mwaka ujao utaongeza kipato chako na kujiwekea akiba.

3. **Tutauza vitu visivyo muhimu**
Je, ulitumia fedha yako ya mkopo kwa vitu visivyohitajika? Je, unakitu chochote katika nyumba yako unachoweza kuuza ili kulipia deni lako? TAFADHARI USIUZE kitu chochote ambacho ni cha muhimu sana ili kusaidia kipato chako, labda kama kipato chako ni kidogo kuliko riba unayopila.

Pamoja na mwenzi wako

- Omba kwa pamoja
    - Mwombe Mungu alinde moyo wako na kwamba akusaidie kuepukana na tamaa juu ya mali ambayo si ya kwako.
    - Mwombe Mungu kama kuna vitu visivyo vya muhimu katika nyumba yako.
    - Mwombe Mungu akujalie kuwa na ubunifu na hekima ya kulipa deni lako mapema iwezekanavyo.

4. Tutakuwa wabunifu na kufanya mpango wa kuwa na mabadiliko madogomadogo ya kulipa deni.
Tunaweza kuwa na mpango wa mbele, kutumia bajeti yetu kulipa madeni yetu yote kwa wakati kwa njia ya kupunguza sehemu flani katika kile tunachopata lakini pia kutoka katika bajeti zetu za familia.

- Je, ni njia zipi umegundua katika familia yako au familia ya wengine ambazo unaweza kuzitumia kupunguza deni lako?
    - *Mfano: Nunua kiasi kidogo cha biskuti au sukari kwa wiki, panda bustani ya mbogamboga, punguza kuhudhuria katika burudani, tumia usafiri wa jamii kuliko kutumia pikipiki yako binafsi wakati wa kweda kazini au shuleni;*
- Je, ni maeneo yapi umegundua watu wamekuwa wabunifu kupunguza gharama katika biashara zao?
    - *Mfano: Tengeneza mbolea yako badala ya kutumia mbolea ya madukani; tumia chenye gharama ndogo; chenye mvuta na usambazaji rahisi, tumiausafiri wa kawaida badala ya kutumia pikipiki kusambaza bidhaa zako.*

Hebu sasa tuangalie mfano unaoonyesha jinsi tunavyoweka mpango wa mbele kuhusu ulipaji wa deni linalotukabili.

KIKUNDI KIKUBWA CHA KIELELEZO
Maelekezo kwa mwezeshaji: *Andika mifano ya namba zilizoonyeshwa katika visanduku vifuatavyo mbele ya darasa. Kama inawezekana, chora masanduku ya mfano karibu na kila mmoja; nyingine ili waweze kulinganishwa kwa urahisi.*

Maria
Maria na Yohana wanahangaishwa na mikopo. Kila mwaka wanapokea mkopo wenye kiasi cha 4,875,000 Tsh. ambao kila miezi mitano wanapaswa kulipa ya 750,000 Tsh. kulipa deni la mkopo na kiasi cha 375,000 Tsh. kama ribaa. Kila mwaka miezi hiyo 5 kabla ya mavuno wanajikuta wameishiwa fedha na kutafuta mkopo kiasi cha dola 750,000 Tsh. ili kulisha familia hadi kipindi cha mavuno kitakapowadia.
Muainisho wake ni kama ifuatavyo:

Mzunguko wa deni la jipya:	
Kipato	4,875,000
- Marejesho ya Mkopo (5m)	750,000
- Malipo ya riba	375,000
- Matumizi yote ya nyumbani	4,500,000
= Jumla (Mkopo unaotakiwa)	-750,000

Siku moja Dorca aliwaatembelea Maria na Yohana. Lengo lake lilikuwa ni kuwasaidia Maria na Yohana kutengeneza bajeti na kufikiri jinsi fedha ilivyokuwa imetumika. Baada ya kuipitia baje ti yote, Maria alipenekeza kupunguza gharama za chakula kwa asilimia 25,000 kila mwezi. Itamghariku lakini walipanda mbogamboga na kufuga kuku wao kidogokidogo na mwisho wakafaulu. Kwa siku iliingia 750 Tsh.lakini Maria alikubali kujaribu.Dorca aliwashauri kuwa itawagharimu lakini bado ni heri kuwa na uhuru wa kifedha. Mnyumbulisho kwa mwka wa pili utakuwa kama ifuatavyo:

Mwaka wa 1	
Kipato	4,875,000
- Marejesho ya Mkopo wa (Mwisho)	750,000
- Malipo ya Riba	375,000
- Matumizi yote ya nyumbani (gharama zilizopunguzwa)	4,200,000
= Jumla (Mkopo unaotakiwa)	-450,000

Ukishamaliza kwa mwaka wa pili, utaona mnyumbulisho ufuatao:

Mwaka wa 2	
Kipato	4,875,000
- Marejesho ya mkopo (mwaka wa mwisho)	450,000
- Malipo ya Riba	180,000
- Matumizi yote ya nyumbani (gharama zilizopunguzwa)	4,200,000
= Jumla (Hakuna mkopo unaotakiwa)	-45,000

HAKUNA MKOPO UNAOHITAJIKA. Katika mwaka wa pili, tayari Maria yuko huru kifedha. Hahitaji kuchukua mkopo. Jambo zuri zaidi ni kwamba, mwaka ujao atakuwa na fedha ya akiba atakayoitumia kununua vitu vya ziada. Hata kama ataongeza matumizi yake na kuwa dola 1,800 bado atakuwa na akiba ya dola 150 kama ziada. Na ikiwa atatumia fedha zake kwa hekima anaweza kuwa na fedha nyingi kwa baadaye.

Mwaka wa 3	
Kipato	4,875,000
- Marejesho ya mkopo (mwaka wa mwisho)	
- Malipo ya Riba	
- Matumizi zote za nymbani (gharama zilizopunguzwa)	4,500,000
= Jumla (Hakuna mkopo unaotakiwa)	375,000

- Dorca alimsaidiaje rafiki yake Maria?
    - *Alimsaidia kukugundua ni wapi angefanya mabadiliko madogo madogo kwenye matumizi yake ya kila siku- ilikuwa ni 750 Tsh. kwa siku.*
- Tunajifunza nini kutoka kwa Dorca na Maria?
    - *Tunaweza kuondokana na deni kama wakati mwingine tutakubali kupunguza matumizi yetu kidogo kidogo na kisha hicho kidogo kilipie deni.*
    - *Tunaweza kuwa huru mbali na madeni ikiwa tutaweka mpango na kutoa vitu tunavyodhani sisi kuwa ni vidogo lakini kumbe tunalipa deni.*
    - *Tunaweza kuondokana na deni kama tutakuwa tayari kumwuliza rafiki tunaye mwamini atusaidie kupitia bajeti yetu, hili nalo ni jambo zuri.*

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Hakikisha wanakikundi wameelewa jinsi ya kufanya mahesabu kuhusu faida inayotokana na ulipaji wa deni letu kwa njia ya kutoa kidogo kidogo ili kuondokana na deni. Wagawie* ***Mwongozo wa Mwanafunzi****: Jinsi ya kuondokana na deni. Pitia mfano na kisha lenga hatua zifuatazo:*

Hatua ya 1: Hesabu kile unachokipata (Jumla ya Kipato chako baada ya makato)
Hatua ya 2: Toa deni (Marejesho ya Mkopo)
Hatua ya 3: Toa Riba (Malipo ya Riba)
Haua ya 4: Toa gharama zote za matumizi ya nyumbani (gharama za kawaida za kila mwezi uongeze gharama nyinginezo)
Hatua ya 4: Toa Matumizi yote ya (gharama za kawaida za mwezi pamoja na nyingine)
Hatua ya 5: Hesabu ili upate Jumla Kuu.
Kama hitaji lako ni kubwa kuliko kipato chako, basi tofauti hiyo ndilo deni.
Rudia kwa kila mwaka.

KUMBUKA- Kama unafundisha kundi kubwa la watu, si kwamaba kila mtu ataelewa jindi ya kufanya mahesabu haya. Lakini ikiwa wewe ni mkufunzi mwenye uzoefu, unayefundisha Wawezeshaji inaweza kuwa masaada zaidi ukifanya mazoezi ya kutosha ili waweze kuelewa na kisha waweze kulisaidia kundi kupitia mbinu hii. Mazoezi mawili yafuatayo yanafaa kwa wawezeshaji wala siyo kwa Kanisa zima.

Mfano wa 1: Jumla ya Kipato 5,000,000 Tsh., Mkopo 1,750,000 Tsh., Riba asilimia 15%, Matumizi 5,000,000 Tsh. + Riba.

Mwaka wa 1

Kipato	**5,000,000**
Marejesho ya Mkopo	**-1,750,000**
Malipo ya Riba	**-262,500**
Matumizi	**-5,000,000**
Mkopo Mpya	**-2,012,500**

Mwaka wa 2

Kipato	5,000,000
Marejesho ya Mkopo	-2,012,500
Malipo ya Riba	-301,875
Matumizi	-5,000,000
Mkopo Mpya	-2,314,375

Mkopo huendelea kukua mwaka hadi mwaka. Lakini hebu fikiria labda wamepata ushauri na kufanikiwa kupunguza matumizi yao kutoka 5,000,000 Tsh. hadi 4,500,000 Tsh. na kuongeza kipato chao kutoka 300,000 Tsh. hadi 5,300,000 Tsh.

Mwaka wa 1

Kipato	5,300,000
Marejesho ya mkopo	-1,750,000
Malipo ya riba	-262,500
Matumizi	-4,500,000
Mkopo Mpya	-1,212,500

Mwaka wa 2

Kipato	5,300,000
Marejesho ya Mkopo	-1,212,500

Malipo ya Riba	-181,875
Matumizi	-4,500,000
Mkopo Mpya	-594,375

Mwaka wa 3

Kipato	5,300,000
Marejesho ya Mkopo	-594,375
Malipo ya Riba	-89,150
Matumizi	-4,500,000
Jumla Mpya – hakuna deni tena	113,975

Hebu tuangalie mfano mwingine tena. Jumala ya kipato 7,500,000 Tsh., mkopo 3,000,000 Tsh., riba 20%, gharama 7,000,000 Tsh. + riba.

Mwaka wa 1

Kipato	7,500,000
Marejesho ya Mkopo	-3,000,000
Malipo ya riba	-600,000
Gharama	-7,000,000
Mkopo Mpya	-3,100,000

Mwaka wa 2

Kipato	7,500,000
Marejesho ya Mkopo	-3,100,000
Malipo ya riba	-620,000
Gharama	-7,000,000
Mkopo Mpya	-3,220,000

Mkopo unaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Unaonaje ikiwa wange pewa ushuri na kupunguza gharama 500,000 Tsh. kwenye 6,500,000 Tsh.na kuongezeka kwa mapato chao 500,000 Tsh. kwa 8,000,000 Tsh.

Mwaka wa 1

Kipato	8,000,000
Malipo ya Mkopo	-3,000,000
Malipo ya riba	-600,000
Gharama	-6,500,000
Mkopo Mpya	-2,100,000

Mwaka wa 2

Kipato	8,000,000
Marejesho ya Mkopo	-2,100,000
Malipo ya riba	-420,000
Gharama	-6,500,000
Mkopo Mpya	-1,020,000

Jambo tunalolioa hapa ni kwamba, baada ya miaka miwili badala ya mkopo kuongezeka na kufikia 3,820,000 Tsh., umeongezeka na kufikia 1,020,000 Tsh. Je, ni kiasi gani cha riba ungelipia kwenye 3,820,000 Tsh? 3,820,000*20 = 764,000 Tsh. Lakini kwa Sababu ya mabadiliko, sasa unalipa 1,020,000*.20 ambayo ni 204,000 Tsh. Huu ni utofauti mkubwa mno. Hebu tuendelee kujifunza.

Mwaka wa 3

Kipato	8,000,000
Marejesho	-1,020,000
Malipo ya riba	-204,000
Gharama	-6,500,000
Jumala Mpya – Hakuna deni tena	-276,000

Kama hawana deni, basi kwa mwaka ujao itakuwa ni rahisi kwao kujiondoa katika deni.

MJADALA: KWAAJILI YA JAMII YA WAKULIMA

Katika kesi ambazo aina ya pekee ya madeni inakulazimu kuuza mashamba yako mapema, basi ni vizuri umtafute mtu ambaye unamwamini kabisa na ili aweze kazi nao. Chagua shamba ndogo na kuuza ili kuwa na pesa kwaajili ya chakula. Kisha wakati wa mavuno uweze kuvuna shamba kubwa na sio kupoteza fedha juu ya hilo. Nji nyingine, unaweza kupanda sehemu ya shamba lako zao jingine ambalo unaweza kuvuna mapema, kama vile mahindi. Njia hii inaweza kukuongezea kazi zaidi, lakini itkusaidia kuuza hayo mazao badala ya kuuza mavuno yako yote mapema. Kuwa wabunifu.

(Kama uko katika eneo ambalo haiwezekani kwa watu kupata mikopo ya kila mwezi, basi fikiria ni chaguzi upi unaweza kuwasaidia watu kupunguza utumiaji mwingi wa fedha zao kwa kulipa riba ya kila mwaka.

5. Mwombe Mungu akusaidie na uwe na imani kuwa atajibu.

KIKUNDI KIKUBWA CHA MJADALA

Hatua ya mwisho ya kuepukana na deni ni kutafuta msaada wa Mungu.Kwakweli, kama tunatarajia kuupata msaada wake, basi tunpaswa kuishi kulingana na mapenzi yake.

Sikiliza hadithi hii:

> Siku moja mtu mmoja alikwenda kwa jirani yake kuomba msaada juu ya deni alilokuwa nalo. Alikuwa amekopeshwa 6,250,000 Tsh. kwa asilimia 10% ya na kuwa baada ya miezi 7 atakuwa amezirudisha kiasi cha fedha 15,000,000 Tsh. Wakati jirani alipohesabu marejesho yake aligundua kwamba idadi ilikuwa mbaya kabisa. Lakini yule mtu hakujua jinsi ya kuhesabu maslahi yake mwenyewe. Mara zote alikuwa anaenda kutoka janga moja la kifedha hadi jingine. Jirani yake alisikiliza hadithi yake ya tatizo la kifedha na kushangaa, "kwa nini Mungu hakumsaidia mtu huyu? Kwa nini yeye daima yuko katika madeni? Je, hii ilikuwa ni kwa sababu ya dhuluma kutoka kwa watu wengine? " Baadaye mtu huyo alianza kueleza jinsi yeye alivyokuwa amekwenda kwa mganga wa kienyeji na kuwa mganga alimwambia kuwa mwaka huo ulikuwa mbaya, ndipo yule mtu akaamini maneno hayo ya mganga wa kienyeji.

Mungu alisema kwamba, ataletea uhaba wa kifedha kwa wale wasiomtii yeye.

- Unadhani mtu huyu alikuwa mtiifu?

Hii ni habari nyingine kutoka katika Biblia:

> Wakati kundi la kwaza la Wayahudi walipoingia Yerusalemu wakitoka utumwani Babeli walianzisha ujenzi wa Hekalu lakini baada ya muda kitambo, walivunjika moyo na hawakuendelea na ujenzi huo tena. Nabii Hagai aliwaonya kwa kuishi katika nyumba nzuri zenye mapambo wakati Nyumba ya Mungu imo katika hali ya kuchakaa. Aliwaonya watu hao tena kuwa hawatatosheka wala hawatabarikiwa maana Mungu hatukuzwi kupitia maisha yao.

Soma Hagai Sura ya 1 na 2:19.

- Je, uhaba wa kifedha ni matokeo ya kutokumtii Mungu?

- *Uhanba wa kifedha wakati mwingine siyo matokeo ya kutokumtii Mungu. Ingawa Daudi alisema kuwa haajawahi kuona mwnye haki akilala njaa. (Zaburi 37:25).*

Changamoto za kifedha muda mwingi ni njia ya Mungu kupima utayari wetu. Tunapokutana na changamoto za kifedha tunapaswa kutulia na kutafakari juu ya maisha yetu, kutubu dhambi zetu na kuomba rehema za Mungu.Ikiwa tutaendelea kuishi maisha ya kutokumtii Mungu, kamwe tusitarajie kupata baraka na rehema zake.

HATUA YA VITENDO

- Kama unadaiwa, basi weka mkakati wa kuyapunguza.
- Panga na familia yako kuhusu mpango huo na kumtia moyo kila mmoja kuhusika.
- Mwombe Mungu akusaidie kupunguza deni na utarajie kuwa atafanya hivyo.

MAPITIO

Tumeagizwa na Mungu tuwe mawakili wema wa fedha.

VIKUNDI VIDOGO

Orodhesha mawazo 10 uliyojifunza katika mafunzo haya.
Je, ni mambo yapi ambayo umeanza kuyafanyia kazi?
Je, ni jambo lipi jingine ambalo umepanga kulifanyia kazi kuanzia muda huu?

Rejesha Ripoti

Mungu hupenda sisi tuufurahie uhuru wa kifedha. Yeye hataki sisi tuwe watumwa wa fedha au wenye mashaka juu ya fedha. Ikiwa tunatumia njia nzuri ya usimamizi wa fedha na kumwomba atupatie maarifa yake na kutusaidia kuujua uhuru.

Fanya maombi ya pamoja ili kuhitimisa.